Ufahamu

# UISLAMU

*Maelezo ya kanuni, maadili na mapokeo yake*

**Ametukuka aliye teremsha Furqani (Qur'ani yenye kutafautisha ukweli na upotofu) kwa mja wake (Muhammad), ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.**

*Qur'an Tukufu 25:1*

# UFAHAMU UISLAMU

*Maelezo ya kanuni, maadili na mapokeo yake*

**Chapisho la 5: Dhu al-Hijjah 1447 / May 2026**

**Haki ya Kunakili**

Islamic Information Center inatoa idhini ya kuchapisha kitabu hiki katika lugha yoyote kwa lengo la kusaidia watu kuufahamu Uislamu, **kwa sharti** kwamba hakitobidilishwa chochote ndani yake, na kadhalika sio kwa lengo la kibiashara.

**Kimeandikwa na Kuchapishwa na**

**Islamic Information Center**
**Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos, Muscat**
**Sultanate of Oman**
**Email: info@iicoman.com**
**www.iicoman.com**




*Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwingi Wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

# YALIYOMO

***Mlango*** ***Ukurasa***


Utangulizi ........ 1
1. Uislamu katika Historia ........ 2
2. Maana ya Uislamu na Kanuni zake za Msingi ........ 8
3. Jinsi na Sifa za Allah – Mwenyezi Mungu Muumba ........ 19
4. Mtume Muhammad – Maisha Yake na Khulka Yake ........ 21
5. Uhalisi wa Mtume ........ 24
6. Historia na Ujumbe wa Qur’ani ........ 30
7. Uhalisi wa Qur’ani ........ 39
8. Desturi na Mafundisho ya Mtume ........ 42
9. Maisha baada ya Kifo ........ 44
10. Mtizamo wa Kiislamu juu ya Dini nyengine ........ 49
11. Yesu katika Uislamu ........ 52
12. Kwanini Uislamu, kwani dini zote si sahihi? ........ 55
13. Hadhari kwa Ukanaji Mungu na Kushuku kuwepo kwa Mungu ... 57
14. Hadhi ya Wanawake katika Uislamu ........ 61
15. Msimamo Mkali wa Kidini na Vurugu ........ 62
16. Jihadi katika Uislamu ........ 64
17. Sharia katika Uislamu ........ 66
18. Mgawanyiko katika Uislamu ........ 68
19. Haki za Mwanadamu katika Uislamu ........ 70
20. Anuwai za Utamaduni katika Uislamu ........ 74
21. Kwanini Dini ni Muhimu? ........ 78
22. Vipi kuingiya katika Uislamu? ........ 80

Orodha ya Maneno ........ 82

Tanbihi ........ 84

Marejeo ya Vitabu ........ 88

# Utangulizi

Allah amewaumba wanaadamu kwa lengo moja tu nalo ni la kumuabudu Yeye na kwa kuishi kwa kuambatana na maamrisho Yake. Kwa muradi huo ameweka dini Yake, Islam. Hili ni neno la Kiarabu lenye maana ya 'kujisalimisha kwenye amri za Mwenyezi Mungu'. Na ameleta watume na vitabu vilivyoteremshwa kuwaongoza wanaadamu kwenye dini hii. Kwa hivyo wanaadamu wote wanayo haki ya kuijua dini hii ya Mwenyezi Mungu, na kupata fursa ya kujiamulia mambo muhimu ya imani na dini kwa ujuzi. Lakusikitisha ni kuwa tangu mwanzoni Uislamu ulitiwa uzushi na kupotoshwa na wapinzani wa dini hii, na mwishowe Uislamu ukafahamika vibaya, na haya ikawa kikwazo kwa wenye kutafuta mwelekeo wa dini iliyokuwa ya haki. Na zaidi ya hayo, mengi yanayosambazwa juu ya Uislamu na hao wenye kujiita 'wajuzi', yameingizwa ndani yake chuki zisizokuwa na sababu na mapendeleo ya kidini. Bila ya shaka hakuna dini yoyote ile ambayo waandishi wa kimagharibi waliandika juu yake kwa upotovu zaidi kama walivyo andika juu ya Uislamu. Na katika maandishi yote yalioandikwa katika miaka ya karibuni, machache sana ni yaliyokuwa ya kuaminika na ambayo misingi yake ni ya ukweli na yenye nia ya kuleta mafahamiano badala ya mafarikiyano na upinzani.

Lengo la kitabu hichi ni kuidhihirisha dini hii kuu na kuondoa yale ya uzushi na mtizamo mbaya juu yake ili kuwapa wanadamu wote fursa na uwezo wa kuuona Uislamu katika sura yake halisi na ya kweli, na kuwawezesha kuona njia sawa itowapeleka kwenye imani ya haki. Mara nyingi imani hutokana na mila za watu, kwa hivyo njia ya pekee ya mtu kutambua ukweli halisi uko wapi ni kuwa na elimu na maarifa ya dini.

# Uislamu katika Historia

Uislamu ni dini na ni utamaduni, uhakika uliosambaa sehemu zote za ulimwengu tokea karne kumi na nne zilizo pita. Uislamu umechangia sehemu kubwa katika maendeleo ya ustaarabu ulimwenguni, hasa ustaarabu wa kimagharibi, na umebadili maisha ya watu wengi kote duniani. Duniani leo karibuni watu bilioni mbili kutoka asili tafauti za kikabila, makundi na utamaduni ni Waislamu halisi. Athari ya Uislamu inaonekana wazi nchi za Magharibi, Asia na Africa. Kwa sababu hii, elimu ya Uislamu ina umuhimu mkubwa kwa wale wenye kushughulishwa na hali ya ulimwengu wa sasa na wale wanaofuatilia elimu na tamaduni katika historia ya Kimagharibi, na kadhalika wale wanaojali uhakika wa kuwepo dini na imani.

Kuufahamu Uislamu vilivyo, lazima mtu afahamu umuhimu wa fikra ya Umma katika Uislamu. Umma wa Kiislamu ni jumla ya Waislamu wote duniani waliofungamana na ujumbe wa Qur'ani wa upweke wa Mwenyezi Mungu na Utawala Wake, ujumbe wa Mtume Muhammad, (Salaa na amani za Allah zimfikiye)[1], na kuikubali na kufwata Sharia ya Mwenyezi Mungu. Ufungamano huu wa nguvu wa Waislamu unadhihiri juu ya misukosuko inayo wapitiya baadhi ya jamii za Kiislamu. Ijapokuwa Waislamu hawana tena muungano wa kisiasa, lakini ni jamii moja ya kidini. Hakuna kikundi chochote cha kikabila duniani kisichokuwa na wafuasi wa Umma wa Kiislamu. Tangu mwanzoni Uislamu imekanusha kwa nguvu sana kila aina za ubaguzi, mgawanyiko na ukabila. Matokeo yake ni kuwa Umma wa Kiislamu umejengeka na vikundi vyote vya kabila zote duniani na kutandaa bara zote za dunia: Asia, Africa, Uropa, Kaskazini na Kusini ya Amerika na Australia.

Historia ya Uislamu haitengeki na historia ya jamii ya Kiislamu, vyuo vake vya elimu na utamaduni wake. Toka kuhama kwa Mtume kutoka Makka kwenda Madina, na kuasisi jamii ya mwanzo ya Kiislamu hapo Madina, mpaka kufa kwake na utawala wa makhalifa wane wa mwanzo

walio na uongozo sahihi (622 CE hadi 661 CE) ni wakati pekee katika historia ya Kiislamu. Ni kipindi cha mfano bora ambacho Waislamu wamekitegemea kwa kupatia uongozo katika historia yao iliyofuata.

Mtawala aliofwatia makhalifa wane wa mwanzo aliimarisha taifa kubwa, na Damascus kuwa ni makao yake, lakini mtawala huyu pia alianzisha ufalme wa urithi. Umayyad ni watawala wa mwanzo wa urithi katika Uislamu, na waliweza kutawala kutoka Asia ya kati mpaka Spain na Ufaransa. Umayyad waliasisi nidhamu ya mawasiliano, nidhamu za serekali, na vyuo vya sharia na vya kijeshi, maendeleo haya yote yalidumu karne nyingi. Mabadiliko mengi yalianzishwa kwenye maeneo ya utawala wao; nidhamu na uwendeshaji wa biashara, kilimo, huduma za posta na huduma za kijamii. Utawala wa Umayyad ulikuwa katika kilele pale walipofanya uamuzi mkuu wa kukifanya Kiarabu lugha rasmi ya ulimwengu wa Kiislamu na kuanzisha na kuchapa sarafu zao wenyewe za dhahabu na fedha. Msikiti wa Umayyad uliopo Damascus na Msikiti wa



*Kasri ya Alhambra Granada, Spain*

Kuba katika Jerusalem (Dome of the Rock) ni miongoni mwa uhodari muhimu wa Umayyad katika fani ya ujenzi.

Katika mwaka 750 utawala wa Umayyad ulipinduliwa na kuchukuliwa na utawala wa Abbasid ambao waliyahamisha makao makuu ya Uislamu na kuyapeleka mji mpya wa Baghdad. Wakati wa utawala wa Abassid ni kipindi ambacho ustaarabu wa Kiislamu ulifikia kilele chake. Watawala wa Abbasid walikuwa wafadhili wakubwa katika fani, sayansi na falsafa, na ni katika wakati huu ndio sayansi ya Kiislamu na falsafa zilistawi. Abbasid waliimarisha mila ya utaalamu ambayo ilishindana na ustaarabu wa Wayunani na Warumi. Na wakati ulipoendelea, kituo cha uongozi wa ilimu cha Baghdad kikasambazika na kuinua vituo vipya huru venye nguvu na usomi mote katika ulimwengu wa Waislamu, ambapo vikachipuka vyuo vya elimu na utafiti viloshindana kwa ubora. Wenye kutafuta elimu kutoka ulimwengu mzima unaojulikana wakati huo walinufaika kwenye vituo hivyo, kama Baghdad, Damascus, Bukhara, Cairo, Fez, Cordoba, Shiraz na nyenginezo. Vigogo vya elimu, kama al-Kindy, al-Farabi, Ibn Sina, Ibn Rushd, Ibn al-Haytham, al-Biruni, al-Khawarizmi na wengi wengine waling'ara kama nyota kwa fikra mpya mpya walizo nazo. Harakati nyingi za falsafa, elimu ya nyota, uganga, hesabu na sayansi ya aina mbali mbali zilikuwa zikitendeka katika ulimwengu wa Waislamu na zilikuwa katika lugha ya Kiarabu – lugha ya ulimwengu ya kutafuta elimu wakati huo. Na ni katika wakati huu upangaji mfumo wa Sharia ya Kiislamu uliyoanzwa na Umayyad ulikamlishwa na kuandikwa rasmi. Pia wakati huu kuliasisiwa vyuo mbali mbali vya Sharia kama vinavojulikana sasa (vyuo vya Kisuni, Kishia na Kiibadhi), na pia kuasisiwa mikusanyo ya Hadithi kamilifu na rasmi za Bukhari, Muslim na wengineo. Miji ya Baghdad na Cordoba ya karne ya tisa na kumi ilikuwa ni maajabu ya dunia – miji yenye ustaarabu wa hali ya juu na mvutio kwa wenye akili za maarifa na za kimila. Watawala wa Ufaransa, Uingereza au Italia wanapotaka mnasihi, mganga wa upasuaji, msanii wa ujenzi au hata

mwana muziki na mshoni, basi huwafatia Baghdad au Cordoba. Miji ya Waislami ilijengwa kwa majumba ya mawe na makasri, mitaa ilikuwa na taa, mifereji ya maji, vyuo vikubwa na maktaba, hospitali na maduka ya dawa, maonyesho ya fani na sehemu za kukoga kwa watu wote. Waislamu wa wakati huo walikuwa wakitumia bidhaa za kisasa za usafi wa kimwili kama sabuni, urembo na manukato. Hakika kipindi cha Abbasid kilikuwa cha ustawi mkubwa (Golden Age) kwa Waislamu kwa upande wa sayansi na uvumbuzi, maisha mazuri na jamii ya kisasa.

Kidogo kidogo nguvu za ufalme wa Abbasid zikaanza kumumunyuka na hatimae kumalizwa na kuchukuliwa na utawala wa Ottomans (Waturuki) katika mwaka wa 1517. Utawala wa Ottomans ulifikia kilele chini ya uongozi wa Sultan Suleiman, anaejulikana kwa jina la umaarufu 'Sultan Suleiman the Magnificent'. Makao yake ya utawala yalikuwa kwenye mji wa Byzantium wa Constantinople (sasa uitwao Istanbul). Wakati alipofariki, nchi zote za Syria, Misri, Afrika ya Kaskazini, Uarabuni na sehemu nyingi za Uropa ya Mashariki zilikuwa chini ya utawala wake. Kwa hivyo Ottomans walikuwa na utawala wa eneo kubwa sana na walilohukumu kwa nidhamu ya kiserekali rasmi na madhubuti ambayo haikuwepo katika dola zozote za wakati ule. Ottomans hawakuzilazimisha eneo hizo mbali mbali za utawala wao kufuata mila moja. Walikuwa wenye kufahamu na wenye kutambua wingi wa utamaduni na tafauti za watu. Waliweka muendesho ambao ndani yake makundi mbali mbali yakaweza kuishi pamoja kwa usalama, na kila kikundi kuachiwa kufuata imani yao wenyewe, mila, sharia na utiifu kwa wafuasi na viongozi wake. Ottomans waliweza kuasisi na kuendeleza utawala uliodumu na uliofuzu kwa kitambo cha karne sita. Karne ya kumi na saba mpaka ya ishirini uliingia na kusambaa ukoloni wa Kiuropa, wakati ambao wafanya biashara wasiokuwa wa Kiislamu, wamishonari, askari jeshi na wasimamizi wa kikoloni waliingia na kutawala nchi nyingi za Waislamu. Wareno,Waspania Wajarumani, Wangereza na Wafaransa wote waliingia

katika kueneza utawala wa kikoloni. Pia Wachina na Warusi wakayapanua madola yao kwa kumeza maeneo yenye jamii kubwa ya Waislamu. Utawala huo wa kigeni sio ulikuwa tu wenye kudhalilisha kwa Waislamu wengi bali ulihatarisha msingi wenyewe wa jamii ya Kiisalmu hapo watawala wa Kiuropa walpoanza kuvigeuza vyuo vya Waislamu vya utamduni, vya sheria na vya serikali kuwa vya Kimagharibi. Wazungu walidhoofisha maadili ya kidini katika nchi za Waislamu kwa kuleta na kupendela athari za Kikristo, mavutio ya kidunia na uthamini wa mila ya mambo ya kidunia. Ilipoingiya karne ya ishirini kipande kidogo tu cha utawala wa Ottomans kiliweza kubakiya mpaka waliposhindwa na kuondolewa baada ya vita vikuu vya kwanza vya dunia. Baada ya kuanguka kwa utawala wa Ottomans, ikaundwa Jamhuri ya Turkia ambayo ilichukuwa siyasa za kiserekali za Kimagharibi. Na nchi zilizobakia ambazo zilikuwa chini ya Ottomans zikapata uhuru wake.

Leo Waislamu wengi wanaendelea kuishi ulimwenguni wakiwamo katika mila zao, juu ya ushambulizi wote ule unaotendeka dhidi ya imani na mtizamo wao wa kitamaduni. Ili kuufahamu Uislamu leo, ni muhimu kwanza kutambua kuwa historia za dini mbali mbali hazikupitia njia moja. Ukristo ulipitia harakati za marekebisho (Reformation movement) katika karne ya kumi na sita na natija yake ni kuja kundi la Protestanti. Uyahudi nao ulipitiwa na marekebisho na kuchipuka kwa vyuo vya kanuni za kale. Lakini Uislamu haukuyapitia hayo, wala hakuna dalili ya kuwepo hata chembe ya namna ya mabadiliko hayo, si kwenye sharia wala sio kwenye mambo yoyote ya dini. Maisha ya kidini na mawazo yake yamebakia pakubwa katika mfumo wa imani sahihi na mila asli. Dhahiri ya kisasa na huo uitwao msimamo mkali (fundamantalism) ambao unaonekana katika vikundi fulani vya jamii ya Kiisalmu na katika nchi fulani vimesababishia maisha ya desturi ya Waislamu kufifia kidogo, lakini pia havikuweza kuleta fikra za sharia na dini za kuzipa changamoto zile za jadi zilizowekwa wakati wa Mtume na wakati wa khalifa wanne

walio na muongozo sahihi. Wingi mkubwa wa Waislamu wanaendela kutekeleza ibada ya jadi iliyoelezewa mwanzoni, na nyendo za maisha yao zinafata Uislamu kama unavyofahamika kijadi. Zaidi ya hayo, ufahamu wa jadi wa Waislamu juu ya Qur'ani, Hadithi, Shari'ah na mengineo unaendelea kama ulivyokuwa karne zote zilizopita, juu ya uharibifu ulioingizwa katika elimu ya jadi ya Kiislamu na nidhamu zake za kisheria.



*Ka'bah iliyopo Makka, ni nyumba ya mwanzo kujengwa katika dunia kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Allah. (Qur'ani 3:96)*

# Maana ya Uislamu na Kanuni zake za Msingi

Dini ya **Uislamu** ni kuamini Upekee wa Mwenyezi Mungu Muumba – Allah, na kuikubali kamili na kutii Amri Yake kama alivyomteremshia mtume Wake wa mwisho, Muhammad, (Salaa na amani za Allah zimfikiye).

Kwa hivyo maana ya Uislamu ni kujisalimisha na amri na matakwa ya Allah kwa hiari na dhati. Kujisalimisha huko humleteya mtu moyo wa ibada, unyenyekevu na uchamungu juuya Mwemyezi Mungu Muumba. Hii ndio hali ya kweli ya kumfanya mtu awe katika amani na Mwenyezi Mungu, amani ya nafsi, na amani kwa viumbe vengine. Wale wanaoamini na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kufuata dini ya Kiislamu wanaitwa **Waislamu**.

Uislamu sio dini mpya. Ni dini ile ile iliyoteremshwa kwa wahyi kwa watume wote wa Mwenyenzi Mungu, kutoka Adam mpaka Núh, Ibrahim, Ismael, Is'haaq, na pia Musa, Issa (Yesu), na mwishowe Muhammad, Salaa na amani za Allah ziwafikie wote. Watume wote hao walikuwa Waislamu kwa sababu wote walikuwa wakimuabudu Allah pekee na walijisalimisha kwa amri zake tu[2]. Vivyo hivyo, watu wote waliokuwa wakiifata dini iliyohubiriwa na watume wote wa Mwenyezi Mungu wanatambulika kuwa ni Waislamu. Kwa maana na ufahamu huu wa neno 'Uislamu' ndio Allah anasema katika Qur'ani (3:19);

***Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu.***

Uislamu umejengeka kwa **Nguzo Sita za Imani** (*Imaan*) na **Nguzo Tano za Dini** (*Islam*). Imani ni kule kuamini kwa uthibitisho moyoni, na dini ni uhakikisho wa imani kwa matendo. Uislamu unahisabia kuwa sharti ya kuwa na dini ni imani, yaani lazima uwe na imani kabla ya dini. kwa sababu imani ni kutambua na kukiri kuwepo kwa Muumbaji na Uungu Wake, Utawala Wake na Haki ya Kuabudiwa. (Kwa Kiarabu *Uluhiyya, Rububiyyah* na *Ubudiyyah*).

# Nguzo Sita za Imani

Nguzo za imani zimetajwa katika aya mbali mbali za Qur'ani[3]. Kwa mfano, kuhusu nguzo ya kwanza Allah anasema katika sura ya 112:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ * اللَّهُ الصَّمَدُ * لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ * وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

***Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwingi Wa Rehema Mwenye Kurehemu***

***Sema: Yeye Mwenyezi Mungu Mmoja (tu). Mwenyezi Mungu Mkusudiwa wa Pekee (kwa ibada na kutegemewa). Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana Naye hata mmoja.***

**Nguzo ya Kwanza**

Kuamini kuwa hakuna mungu apaswaye kuabudiwa ispokuwa Allah. Yeye Ndiye Muumbaji wa ulimwengu, ni Mmoja na Pekee, sifa zake ni pekee na haiwezekani kuwepo na washirika Naye. Imani hii inaitwa *Tawheed* kwa Kiarabu.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *(a) Upekee wa Muumbaji una maanisha upekee wa lengo katika kuumba, na hii ina maanisha upekee wa dini, ambayo ni njia ya pekee ya maisha. Wanadamu wengi wamo katika kuhangaika na kutapatapa kiroho na kutokuwa na utulivu wa moyo kwa sababu ya kukosa lengo thabiti la maisha. (b) Kuzipachika sifa za Mungu kwa viumbe vyengine kunazua imani potofu, ambayo inaleta hofu, ufisadi na unyonyaji.*

**Nguzo ya Pili:**

Kuamini kuwepo kwa Malaika, ambao ni watumushi na wawakilishi wa Allah. Kinyume na wanadamu, umbile la Malaika ni la kiroho, na hawana kiwiliwili. Wameumbwa kuwa daima katika hali ya kumuabudu Allah na kutekeleza maamrisho Yake.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *Kuamini mambo tusioyaona na yaliyo nje ya upeo wa hisia za kiwiliwili cha mwanadamu ni moja katika masharti ya imani. Nguzo hii inauongezea zaidi uwezo wa akili ya mwanadamu kutambua na kufahamu maumbile yaliyopita kikomo cha hisia za viwiliwili vyetu, na kutufungulia njia ya kuwa na fahamu ya mambo ya kiroho.*

**Nguzo ya Tatu:**

Kuamini vitabu vyote walivyoteremshiwa watume wa Allah. Kwa mfano, Zaburi (*Psalms*) aliyoteremshiwa Daud, Taurati (*Tora*) aliyoteremshiwa Musa, Injili (*Gospel*) aliyoteremshiwa Issa (Yesu), na Qur'ani, aliyoteremshiwa Muhammad, Salaa na amani za Allah ziwafikie wote.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *Nguzo hii ni hoja ya kiakili kwa sababu vitabu vyote vimekuja kutoka kwa yule yule Mwenyezi Mungu Muumba, vikiwa na msingi uleule wa imani na mfumo wa maadili uleule. Itakuwa ni kinyume kukubali kitabu kimoja na kuvikataa vyengine. Pia haiingii akilini kuwa Mwenyezi Mungu Muumba atateremsha kwa wanadamu ujumbe tafauti na wenye kupingana. Qur'ani inathibitisha vitabu vilivyopita, inakamilisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wanadamu na inasahihisha mabadiliko yaliyofanywa na watu katika huo ujumbe wa kale ambao unachukuliwa sasa na baadhi ya watu kuwa ni ujumbe wa watume wa mwanzoni.*

**Nguzo ya Nne:**

Kuamini kwa watume wote wa Allah kutoka Adam mpaka mtume wa

mwisho Muhammad, Salaa na amani za Allah ziwafikie wote.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *Nguzo hii pia ni hoja ya akili kwa sababu watume wote wametokana na Mwenyezi Mungu Muumba mmoja, na wamekuja na ujumbe mmoja kwa wanadamu. Kukubali mtume mmoja na kukataa wengine si kinyume tu bali huleta mgawanyiko wa dini ya Mwenzi Mungu.*

**Nguzo ya Tano:**

Kuamini kuwepo kwa Siku ya Hukumu (Malipo). Wanadamu, sio kama Malaika, wamepewa uhuru wa kuchagua: Anaweza mtu kuchagua kufuata maamrisho ya Allah, au anaweza kuchagua kutokutii. Lakini uhuru huu una jukumu na kuhesabiwa kwa Allah. Siku ya Hukumu tutawajibika kuhisabiwa katika yale tulioyochagua katika maisha haya. Wale waliochagua sawa na wakafuata ujumbe wa Allah wataingia Peponi milele. Na wale waliokosea katika kuchagua na kupuuza ujumbe wa Allah wataingia Motoni milele.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *Nguzo hii inatuonyesha kuwa tuna malipo kwa Mwenyezi Mungu na malipo kwa yale matendo yetu hapa duniani. Hamu yetu na matarajio yetu ya kupata haki ya kweli na yakuridhisha itapatikana hapo itakapo amuru haki ya Mwenyezi Mungu iliyokamilika na ya kweli Siku ya Hukumu.*

**Nguzo ya Sita:**

Kuamini katika Uamuzi wa Mwenyezi Mungu na Majaaliwa Yake. Kila kinachotokea ulimwenguni (kizuri, kibaya au vyovyote) basi kinatokea kwa njia ya kanuni na kipimo alivyoweka Allah kwa hekima na maarifa Yake yasio na kikomo, (Kwa Kiarabu *Qadha wa Qadar*). Hakuna kilichomo katika Ulimwengu kikawa nje ya kanuni hizi za Allah (za kimaumbile na kiroho) na kipimo cha Allah (kwa ukubwa na wingi). Zaidi ya haya, sio tu kuwa Allah anathibiti Ulimwengu kamili kwa kanuni na vipimo

vyake, bali pia yamo mikononi Mwake maarifa ya kila kitu kilichomo Ulimweguni, na anajuwa na kuhifadhi kila kitu kitokeacho – yaliyopita, ya sasa na yatayotokea siku za mbele. Tunasoma katika Qur'ani (6:59);

> ***Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha.***

Miongoni mwa maarifa ya Allah yaliyo kamili ni kujua kinachoendesha uhai wa mwanadamu, na matokeo na misukosuko ya hali yake. Lakini, huko kujua kwake Allah harakati, matokeo na matendo ya mwanadamu kabla ya kutendwa na kutokea, hakumlazimishi mtu kufanya matendo hayo. Kwa mfano, wanajimu wanaweza kutabiri na kuandika lini jua litapatwa katika miaka ya mbele kwa kutimia elimu yao ya sayansi. Huko kupatwa kwa jua kutatokea sio kwa sababu ya wao kujua na kutabiri. Vivyo hivyo, Allah kwa elimu yake isiyo na kikomo (wala kupunguka kwa sababu ya wakati wala upeo) anajua na kuhifadhi nini wanadamu watakitenda, lakini hii haimaanishi kulazimika kwa mtu kutenda matendo hayo.

Kwa hivyo, hoja hizi zilizoelezewa hazipo kinyume na uhuru wa kuchagua na kitendo ambao amepewa mwanadamu; kinachomaanisha ni kuwa tunayoyafanya na uwezo wa hiari zetu daima zitafuata (a) kanuni alizoziweka Allah, (b) matokeo ya yale tuliyoyachagua yatakuwa kwa kipimo alichokiweka Mwenyezi Mungu, na (c) Allah anajua kabla yale tuliyoyachagua na kuyatenda, lakini jukumu ni juu yetu kwa yale tuliyoyachagua kuyafanya[4]. Vilevile, ijapokuwa wanadamu wana uhuru wa kuchagua na kutenda waliyoyachaguwa, nguvu na uwezo wa kutenda chochote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu Muumba.

***Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya! (Qur'ani 37:96)***

Hii inamaanisha kuwa uhuru wa kuchagua wa mwanadamu ni sharti ya mwanzo ya Dhamiri ya Mwenyezi Mungu na Yeye kuwezesha kitendo cha mwanadamu. Yaani wanadamu wanayataka hayo matendo, na Allah anawatekelezea (ikiwa uamuzi Wake ni kuyatekeleza). Na hivi ndivyo dhamiri ya mwanadamu inavyofanya kazi pamoja na Dhamiri ya Mwenyezi Mungu. Unaweza kusema, majaaliwa ya mema na maovu yote yamo mikononi mwa Allah, lakini, uovu unajaaliwa kutokana na matokeo ya aliyokichagua mwanadamu – yaani, matokeo kwa vile wanadamu kutotumia au kutumia vibaya uhuru wao wa kuchaguwa. Allah Anajaalia matendo na matokeo yake.

***Jema lilio kufikia limetokana na Mwenyezi Mungu. Na ovu lilio kusibu linatokana na nafsi yako. (Qur'an 4:79)***

Kwa upande wa Allah, kujaaliwa kuwepo uovu au kuruhusu uovu utokee sio asili ya kutokea uovu wenyewe, lakini mwanadamu kuchagua maovu ndio uovu. Mwenyezi Mungu hachagui maovu, wanadamu ndio wenye kuchagua maovu.

***Umuhimu wa nguzo hii ya imani:*** *Kuamini kuwa uthibiti halisi na utawala wa ulimwengu wote ni wa Mwenyezi Mungu Muumba, Allah, kunaikaza imani yetu ya Ufalme Wake juu ya ulimwengu. Kwa zile sifa za Allah za Rehema na Ulezi juu ya Ulimwengu Wake, imani hii inaingiza tumaini, usalama wa roho na unaimarisha nyoyo za waumini.*

***Hizi nguzo sita za imani ni chanzo cha kuipa akili ya mwanadamu fahamu kuhusu roho na utambuzi wa mambo ya kiroho. Nguzo hizi vilevile zinafafanua nani "muumini" kwa ukamilifu; Kutokuamini chochote katika nguzo hizi, kama vile kukubali mtume mmoja na kukataa wengine, kunamfanya mtu kuwa "sio muumini".***

# Mwito wa Salaa (*Adhana*)

*Allah ndio Aliye Mkubwa, Allah ndio Aliye Mkubwa,*

*Allah ndio Aliye Mkubwa, Allah ndio Aliye Mkubwa,*

*Nashuhudia kuwa hakuna mungu apaswae kuabudiwa isipokuwa Allah,*

*Nashuhudia kuwa hakuna mungu apaswae kuabudiwa isipokuwa Allah,*

*Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah,*

*Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah,*

*Njooni katika Salaa, Njooni katika Salaa ,*

*Njooni kwenye Mafanikio, Njooni kwenye Mafanikio,*

*Allah ndio Aliye Mkubwa, Allah ndio Aliye Mkubwa*

*Hakuna mungu apaswae kuabudiwa isipokuwa Allah*

*Adhana ni mfululizo wa ukumbusho kwa wanadamu kwamba hakuna mungu apaswae kuabudiwa isipokuwa Allah, na Muhammad ni mtume wa Allah.*

# Nguzo Tano za Dini

Nguzo tano za dini zimeandikwa katika aya kadha za Qur'ani[5]. Kwa mfano, kuhusu nguzo ya kwanza, Allah anasema katika Qur'ani aya 49:15

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

***Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli.***

**Nguzo ya Kwanza:**

Kukiri ndani ya moyo na akili kuwa hakuna mungu anaepasa kuabudiwa isipokuwa Allah, na Muhammad ni mtume wa Allah. Kukiri huku kunathibitisha imani ya mtu katika Upekee wa Muumbaji na kuwa Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) ni mtume wa mwisho wa Allah. Nguzo hii kwa kiarabu inaitwa *Shahadah*, na maana yake ni kushuhudia, kushikilia na kuusimamisha ukweli uliodhihirishwa.

Baada ya kukiri imani yake, Muislamu anawajibika kuikamilisha imani yake kwa vitendo vilivyo amrishwa katika nguzo zifuatazo.

**Nguzo ya Pili:**

Kufanya ibada ya salaa mara tano kwa siku; alfajiri, adhuhuri, laasiri (jioni), magharibi na usiku. Salaa ni mawasiliano yetu moja kwa moja na Allah, bila kuwepo na mwakilishi kati yake, na inahusika na kumtukuza na kumsifu Allah na pia kufikisha maombi (dua) zetu kwake.

***Umuhimu wa nguzo hii ya dini:*** *Salaa, kama alivyo ieleza Allah, ni njiya ya kumkumbuka Allah na njiya kujikinga na maasi (Qur'ani 20:14 na 29:45). Kwa hivyo hizi salaa za mara kwa mara zinatusaidia kuikuza na kusisitiza hisia na unyenyekevu juu ya Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo zetu. (kwa Kiarabu, taqwa [6]).*

**Nguzo ya Tatu:**

Kutoa msaada kuwapa masikini na wenye kuhitaji (kwa Kiarabu *Zakah*). Muislamu anatakiwa kutoa asili-mia 2 ½ (2.5%) ya mali yake ambayo hakuitumia katika mwaka mzima uliopita, kama vile akiba ya pesa, fedha na dhahabu. Kulipa *Zakah* inwajibika pia kwenye mapato ya kilimo, hisa za kibiashara na kadhalika.

***Umuhimu wa nguzo hii ya dini:*** *Nidhamu ya Zakah inahakikisha kuwa mali yanasambazwa katika jamii ili kuondowa umasikini, wivu na uhasama katika jamii. Neno la 'Zakah' lina maana ya 'kutakasisha', kwa hivyo kwa Rehema ya Allah Zakah inatakasisha mali yetu na nyoyo zetu.*

**Nguzo ya Nne:**

Kufunga tokea panapokucha mpaka linapotua jua kila siku katika mwezi wa *Ramadhani*, ambao ni mwezi wa tisa katika takwimu ya Kiislamu. Wakati wa mchana ni lazima kwa Muislamu kujizuwia na kula, kunywa na vitendo vya kijinsi, na pia kujizuwia na yote yaliyokatazwa katika dini kama vile kumsema mtu, kushuhudia kwa uongo na kadhalika.

***Umuhimu wa nguzo hii ya dini:*** *Kufunga ni mazoezi yanayomsaidia mtu kukuza na kuimarisha nguvu ya kiroho, uvumilivu, na haya huzidisha imani, hisia na unyenyekevu juu ya Mwenyezi Mungu ('taqwa' kwa Kiarabu). Funga pia inatusaidia kuwakumbuka watu wasio bahatika na yale tuliyonayo; watu ambao hata chakula kimoja cha siku kukipata kwao ni tabu..*

**Nguzo ya Tano:**

Kwenda hija Makka (kwa kiarabu *Hajj*), mara moja katika maisha ya mtu kwa wale wanaojiweza kwa hali na mali.



***Kituo cha Ibrahim (Maqaam Ibrahim) katika Makka, mahala ambapo Ibrahim (salama na baraka za Allah zimfikie) alisimama wakati akijenga Kaaba.***

***Umuhimu wa nguzo hii ya dini:*** *Hija ni mkusanyiko mkubwa wa Waislamu kutoka sehemu zote za ulimwengu. Nayo ni uthibitisho na maonyesho ya umoja wa wanadamu na umoja wa dini; Mwenyezi Mungu ni Mmoja, wanadamu ni kitu kimoja na dini yao ni moja. Hija ni aina ya ibada na kumtukuza Allah, na pia ni kumbusho la ibada na mhanga waliojitolea Mtume Ibrahim na mwanawe Ismail, salama na baraka za Allah ziwafikie.*

***Nguzo hizi za dini zinatusaidiya kutengana na mahitajio ya kiwiliwili na ya kidunia na kuikuza nguvu na hisia ya kiroho. Yaani zinatunyanyua kutoka kwenye mwelekeo wa kidunia na kutuweka kwenye mwelekeo wa kiroho, ambamo kwa mfululizo tunakuwa na hisia ya kuwa na Mwenyezi Mungu Muumba, utumikaji na uwajibikaji wetu Kwake na jukumu letu kwa wanadamu.***



***Sura ya mnara katika Msikiti Mkuu wa Sultan Qaboos Muscat, Oman. Minara katika zama zilizopita ilikuwa ikitumika kwa kusambaza sauti ya adhana. Sasa hutumika zaidi kuwa ni alama ya msikiti.***

## Jinsi na Sifa za Allah – Mwenyezi Mungu Muumba

Kama vile kila mtu huwa na jina, basi pia Muumbaji na Bwana wa Ulimwengu anajulikana kwa jina lake la "**Allah**". Jina hili ni la pekee lisilo na jinsi, wala wingi, na nila asili. Allah sio mwanamme wala sio mwanamke. Hatokani na baba wala mama. Hakuna wa pili kama Yeye au katika mfano Wake, hakuna alie sawa Naye au kifani Naye. Cheo Chake kipo safi kabisa na bila ya mshirika, Yeye ni Mmoja Pekee anayestahiki kuitwa kwa jina la **Al-Wahid**, Mmoja na Pekee asiyekuwa na kifani. Kwa hivyo:

1. a) Allah ana sifa za kupita uwezo wote wa alivyoviumba, kama kuwepo kwake bila ya kutegemea chochote, hana chanzo wala hana mwisho na kadhalika, (b) Allah ana sifa za pekee za kutolingana na chochote katika alivyoviumba. Kwa mfano, Yeye pekee mwenye uhai wa daima na Mwenye kuleta uhai, Mwenye Kusikia yote, Mwenye Kuona yote na ni Mwenye kuziwezesha hisia hizo, Mwenye Nguvu Zote na Mwenye Uwezo wa kutekeleza Atakayo, na kadhalika. Sifa zote hizi ni za pekee na hazina mshiriki yoyote.

2. Allah ni mwenye majina mengi mazuri ambayo yanatokana na Sifa Zake. Miongoni mwa hayo ni Mwingi wa Rehema, Mwenye Kusamehe, Mwingi wa Huruma, Mwenye Hekima na kadhalika.

3. Uungu wa Allah, Utawala na Haki ya Kuabudiwa (kwa Kiarabu *Uluhiyyah, Rububiyyah* na *Ubudiyyah*), sifa zote hizi hazina mshiriki yoyote.

4. Kwa Utukufu huu wa Mwenyezi Mungu, jina la Allah linamaanisha kuwa utiifu na mapenzi yetu kamili yawe kwake yeye tu, na kwake yeye tu panapatikana himaya na pa kukimbilia.

Kufuatana na haya, jina la Allah linabainisha Upekee wa Mwenyezi Mungu Mmoja (monotheism). Na zaidi ya hayo, hii maana nzito ya

jina 'Allah' inalifanya neno 'Mungu' lisitosheleze maana kamili ya 'Allah', ijapokuwa katika fasihi ya Kiislamu maneno yote mawili yanatumika mara kwa mara kwa maana moja.

Kwa vile Allah ndiye Muumba na Mlezi wa Ulimwengu na viumbe vyote vilivyomo, imani yetu Kwake na utiifu wetu Kwake ni uthibitisho wa shukurani zetu Kwake. Kumkataa Allah au kumshirikisha na kiumbe chengine chochote, (*shirk* kwa Kiarabu), ni kosa kubwa la kutomshukuru Yeye, na kwa hiyo inaleta dhambi kubwa kabisa ambayo Allah haisamehe kamwe, ila kwa aliye tubia. Allah anasema katika Qur'ani (4:48);

> ***Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa.***



***Kanisa kuu la Córdoba (Spain) linalojulikana kwa jina la 'Cathedral of Our Lady of the Assumption'. Jengo hili, ambalo ni ufanikisha mkuu wa ujenzi wa Kiislamu, lilikuwa likijulikana kwa jina la "Msikiti Mkuu wa Córdoba" wakati wa utawala wa Waislamu.***

# Mtume Muhammad – Maisha Yake na Khulka Yake

Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) ni mtume wa Allah kwa wanadamu wote. Kabla ya Mtume Muhammad, Allah alituma watume wengi wengine kama Nuh, Ibrahim, Musa na Issa, salama na baraka za Allah ziwafikie. Kila mtume alitumwa kwa taifa maalumu na kwa wakati maalumu. Waislamu wanaamini na wanawapa heshima watume wote wa Allah. Waislamu wanampa Mtume Muhammad heshima ya juu kabisa kwa sababu yeye ni mtume wa mwisho aliyeletwa kwa wanadamu wote kuutangaza ujumbe wa asili kwa walimwengu wote na wakati wote.[7]

**Ukoo wake**

Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alikuwa Mwarabu na anatokana na kizazi cha Ismail mwana wa Ibrahim (salama na baraka za Allah ziwafikie). Anatokana na ukoo wa Bani Hashim wenye heshima kubwa, nao ni mmoja katika koo za kabila la Quraysh katika Makka.

**Kuzaliwa kwake**

Mtume Muhammad alizaliwa Makka katika mwaka wa 570 CE, takriban karne sita baada ya Nabii Issa (salama na baraka za Allah ziwafikie wote). Wazazi wake wote wawili walitokana na kizazi chenye daraja ya juu na wakihusiana. Baba yake alikuwa Abdallah, mwana wa Abd al-Muttalib, mwana wa Hashim, mwana wa Abd al-Manaf, mwana wa Qussay, mwana wa Kilaab, mwana wa Murrah. Mama yake alikuwa Aaminah, mwana wa Wahab, mwana wa Abd al-Manaf, mwana wa Zuhrah, mwana wa Kilaab, mwana wa Murrah.

Baba yake Mtume Muhammad alifariki kabla yeye kuzaliwa, na mama yake alifariki alipokuwa na umri mdogo wa miaka sita tu. Alilelewa na babu yake, Abd al-Muttalib. Baada ya miaka miwili akachukuliwa kulelewa na ami yake Abu Talib, ambaye alichukuwa uongozi wa ukoo

wa Bani Hashim baada ya kufariki Abd al-Muttalib.

**Khulka na tabia yake**

Kabla ya kupata utume, Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alinyanyukia kuwa mtu mnyenyekevu, mwema na mwenye tabia njema ya maadili. Hakuwa mtu aliyesoma na hakupata kamwe kuabudu masanamu, wakati ambao ibada ya masanamu ilikuwa ni mwendo wa watu wake. Badala yake alikuwa akijitenga kwa masiku na kukaa katika pango liliopo karibu na Makka, kutafakari juu ya Muumba na viumbe Vyake.

Alikuwa akijulikana kwa jina la 'mkweli na muaminifu' (kwa Kiarabu *As-Saadiqul-Ameen*), na alikuwa mwenye uaminifu mkubwa. Watu wengi walikuwa wakiaminisha kumpa amana zao kwa ajili ya biashara au kudhihifadhi.

Mtume Muhammad alikuwa akijali hali ya watu wake kwa kuwatetea masikini na wasiokuwa na uwezo, na kushirikiyana na jumuiya zenye kuwasaidiya.

**Kuteremshwa Wahyi**

Katika moja ya siku alizokuwa akijitenga katika pango, Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alipokea wahyi wa mwanzo kutoka kwa Allah kwa njia ya Malaika Jibril:

> ***Soma kwa jina la Mola wako Mlezi aliye umba, Amemuumba binaadamu kwa tone la damu, Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyo kuwa hayajui (Qur'an 96:1–5).***

Wahyi huu wa mwanzo uliteremka katika mwaka wa 610 CE wakati Mtume Muhammad akiwa na umri wa miaka 40.

***Wahyi huu wa mawanzo unadokeza kuwa elimu na kutafakari ni msingi wa kuhubiri imani, na kwa hakika ni msingi wa imani yenyewe.***

Wahyi uliendelea kuja kwa njia ya Malaika Jibril kwa miaka 23 mengine iliyofuata katika maisha ya Mtume. Katika miaka 13 ya mwanzo aliutangaza ujumbe wa Uislam katika Makka, ambapo yeye na wafuasi wake walikabiliwa na upinzani mkubwa na hata kuadhibiwa. Lakini katika mwaka wa 622 CE, kwa vile kuadhibiwa kulizidi na kufululiza, Mtume na wafuasi wake wakalazimika kuhamia Madina, mji ambao upo karibuni kilomita 400 kaskazini ya Makka. Watu wa Madina waliwapokea kwa heshima na ukarimu mkubwa. Mtume aliendelea kupokea na kutangaza Ujumbe wa Allah katika mji wa Madina kwa miaka 10 iliyofuata, ambapo pia alianzisha serekali ya Kiislamu.

**Kufa kwake**

Mtuma Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alifariki katika mwaka wa 632 CE akiwa na umri wa miaka 63 baada ya kuumwa kwa muda mfupi, na akazikwa Madina katika nyumba ya mkewe Aisha, (Radhi za Allah zimfikie).

***Basi mtegemee Mweneyezi Mungu; hakika wewe uko juu ya Haki iliyo wazi. (Qur'an 27:79)***



# Uhalisi wa Mtume

Katika historia yote ya mwanadamu, uhalisi wa watume wote wa Mwenywzi Mungu ulikuwa daima ukitiliwa shaka, na kwa Mtume Muhammad pia haikuwa tafauti. Qur'ani inatueleza kuwa thibitisho la watume wa Mungu limo katika tabia zao njema na katika ukweli usiopingika wanaokuja nao kutoka kwa Mola wao. Kuhusu Mtume Muhammad, kuna hoja nne zenye kuteteya uhalisi wake.

**Hoja ya mwanzo**

Kama tulivyoona katika Mlango wa 4, Mtume Muhammad alikuwa mtu mwenye msimamo thabiti na uadilifu na alikuwa akiheshimiwa sana na watu wake. Hata alikuwa akijulikana kwa moja katika majina yake ya lakabu '*mkweli na muaminifu*'. Mtume alianza ujumbe wa utume akiwa na umri wa miaka 40. Ni jambo lisilo na mantiki na la kuingia akilini kufikiria kuwa mtu mwenye sifa hizo za tabia njema na katika umri huo mkubwa aweze ghafla kugeuka kuwa muongo na laghai.

Anaweza mtu kutoa hoja ya kuwa labda akitaka utukufu katika jamii yake. Lakini tokea hapo alikuwa mtu mwenye kuheshimiwa na akitoka kwenye kabila la Quraysh lenye nguvu na kuheshimiwa katika Makka. Na kwa hakika mwanzoni alipoanza ujumbe wa utume, watu wake walimshawishi kumpa ukubwa ili kumtoa katika fikra ya kutangazia ujumbe wa utume, akakataa katu[8]. Hii inathibitisha kuwa hakuwa akitafuta cheo.

**Hoja ya pili**

Ushahidi wa watume wa Mwenyezi Mungu umo katika ujumbe walioteremshiwa na Mwenyezi Mungu. Ushahidi wa Mtume Muhammad ni Qur'ani. Kama ilivyoelezwa katika Mlango wa 7, haiwezekani kuwa Qur'ani iliandikwa na Mtume; ni yakini kuwa ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hakika mwanadamu amepewa changamoto ndani ya Qur'ani yenyewe kuweza kuleta kitabu cha mfano wake, ikiwa

kuna yoyote alienayo dhana kwa Mtume aliiandika. Na kama ilivyoelezwa kabla, Mtume hakuwa mwana wa chuoni wa kuweza kuandika kitabu kama hicho. Qur'ani ni uthibitisho wa daima wa uhalisi wa Mtume, na ni muujiza wa pekee aliodai Mtume.[9]

**Hoja ya tatu**

Mtume Muhammad , Salaa na amani za Allah zimfikiye, alianzisha harakati ambayo iliubadilisha ustaarabu wa jamii ya mwanadamu kuwa bora kwa njia ya ukamilifu na haraka kushinda harakati zozote za mwanadamu katika historia. Na zaidi ya hiyo, hakuna dini iliyokuwa na athari yenye kudumu juu ya ustaarabu wa mwanadamu na maendeleo yake kama athari ya Uislamu. Si jambo la akili na mantiki kudhani kuwa athari hii kubwa na ya kudumu imekuja kwa sababu ya harakati ilio letwa na kuongozwa na mtu muongo na laghai.

**Hoja ya nne**

Mtume Muhammad, Salaa na amani za Allah zimfikiye, alitabiriwa katika vitabu vya dini zote kubwa: Uyahudi, Umasihi, Uhindu na Ubuda.

Qura'an inatujulisha kwamba Mtume Muhammad alitabiriwa katika vitabu vya Kiyahudi na pia vya Kimasihi.

> ***Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii (Muhammad), asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili. (Qur'an 7:157)***

Katika Kumbukumbu 18:18 tunasoma:

> ***Mimi nitawaleteya nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe (Musa), nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru.***

Hakuna mtume yoyote aliyekuja baada ya nabii Musa ikamuelekea aya hii ya Agano la Mwanzo isipokuwa Mtume Muhammad: **Kwanza**, ndugu wa Wayahudi ni Waarabu. Kizazi cha Israel kinatokana na Is'haaq na kabila la Waarabu linatokana na Ismail. Is'haaq na Ismail ni wana wa Ibrahim na kwa hivyo vizazi vyao vitakuwa ni ndugu. **Pili**, Muhammad anafanana na Musa katika mengi, ambapo Issa (Yesu) hafanani; (1) Musa na Muhammad walikuwa na baba na mama. Issa alikuwa na mama, wala hakuwa na baba. (2) Musa na Muhammad walizaliwa na mama zao kutokana na mimba za kawaida. Mimba aliyozaliwa Issa ilikuwa ya kimiujiza. (3) Musa na Muhammad walioa na wakawa na watoto, hali Issa hakuoa. (4) Musa na Muhammad walikuja na sheria na kanuni kwa watu wao, hali Issa hakuja na hayo. (5) Musa na Muhammad walikufa kifo cha kawaida. Katika imani zote mbili za Kiislamu na Kimasihi, Issa hakufariki dunia kwa njia ya kawaida. **Tatu**, kama inavyotujulisha Qur'ani (53:3-4), Mtume Muhammad hakuwa akisema kwa kauli yake bali maneno yake yalikwa ni ufunuo wa moja kwa moja au wahyi kutoka kwa Mungu.

Tuje katika Agano Jipya, katika Injili ya Yohanna tunasoma:

> ***Ninayo bado mengi ya kuwaambieni, ila kwa sasa hamwezi kuyastahmili. Lakini atakapokuja huyo Roho ya kweli atawaongoza kwenye ukweli wote; maana hatasema kwa mamlaka yake mwenyewe, bali atawaambieni yote atakayosikia, na atasema mambo yatakayokuwa yanakuja. Yeye atanitukuza mimi kwa kuwa atawaambieni yale atakayopata kutoka kwangu. (Yohana 16:12-14)***

Aya hizi zinazungumzia "Roho ya kweli" ambaye hatosema kwa kauli yake, (kama tulivyosoma hapo juu). Haiwezekani kuwa 'Roho Mtakatifu' ni yuleyule 'Roho ya kweli', kwa sababu Roho Mtakatifu tayari alikuwa



*Minara katika anga ya Upande wa Asia wa mji wa Istanbul*

na Issa (tazama Luka 4:1 na 3:22, Yohana 20:22, Matendo 2:4, n.k.). Na zaidi ya hayo, Roho ya kweli itamtukuza Issa. Hakujatokea mtume baada ya Issa aliyemtukuza Issa isipokuwa Muhammad, (tazama Mlango wa 11). Hapana shaka kuwa huyo 'Roho ya kweli' ataekuja baada ya Issa ni Muhammad, salama na baraka za Allah ziwafikie wote.

Na zaidi ya hayo, Mtume Muhammad anatabiriwa katikia Biblia kwenye Isaya 29:12, Yohana 14:16, Yohana 16:7, Mathayo 21:43 and Matendo 3:22. Angalia kwamba neno 'Msaidizi' lililotajwa katka aya hizi za Biblia ni tafsiri ya neno la Kiyunani '*Paracletos*'. Neno hili ni mbadilisho wa neno asili la Kiyunani '*Periclytos*' lenye maana ya 'aliyesifika' au kwa Kiarabu 'Ahmad' au Muhammad'.[10]

Ukisoma kwa utulivu na bila ya kuelemea fikra ya upande mmoja, utaona pia kuwa Mtume Muhammad alitabiriwa katika maandiko ya Kihindu na hata ya Kibuda. Katika kitabu chake chenye jina la "*Muhammad in the Hindu Scriptures*", Dr. Ved Prakash Upaddhay amefukua ndani ya maandiko ya Kihindu ishara nyingi zinomuelekeya Mtume Muhammad. Maandiko ya Kihindu ya 'Vedas' yanaeleza juu ya kuja kwa mtu wa dini na hikma (Sage), ambaye sifa zake zinamuelekea Mtume Muhammad. Sifa zenyewe, ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Sanskrit, ni hizi zifwatazo:

1. *Narashagsa* ambayo tafsiri yake ni 'aliyesifika'. Hii ni maana ya majina yote mawili ya Mtume, Ahmed na Muhammad. Zaidi ya hayo, mahala pa kuzaliwa na sifa za *Narashagsa* zinaelekea kabisa na zile za Mtume.

2. *Antim Rishi* au 'Shehe wa mwisho'. Mtume Muhammad alikuwa ni mtume wa mwisho kwa wanadamu.

3. *Kalki Avatar*, maana yake ni Shehe atayekuja kwenye kizazi cha mwisho. Mtume Muhammad aliletwa kuwa ni mtume wa mwisho kwa wanadamu wote.

4. *Kauram*, yenye maana ya mhamiaji. Mtume Muhammad alikuwa mhamiaji katika Madina. (Tazama Mlango wa 4).

5. Baba yake ametajwa kuwa ni "*Vaishnuvesh*" yenye maana ya 'Mtumwa wa Mungu' na mama yake '*Sumati*' yenye maana ya 'Salama'. Majina haya mawili yanalingana na '*Abdallah*' na '*Amna*' kwa Kiarabu, ambayo ni majina ya baba na mama wa Mtume.

6. Jina la huyo Shehe atayekuja ni *Mamaha*. Hili sio neno la lugha ya Sanskrit bali linaelekea kuwa ni neno la kusukwa ndani ya Sanskrit lenye asili ya Kiarabu ya jina la Muhammad.

Katika maandiko ya Kibuda, Gautama Buddha alitabiri kuja kwa *Antim Buddha* au Shehe wa Mwisho, mwenye jina la Maitreya. (Gospel of Buddha, Carus, ukurasa 217). Maelezo juu ya huyu Maitreya yanaelekea na sifa za Mtume Muhammad:

1. Mtume Muhammad alikuwa ni mtume wa mwisho, 'Shehe wa Mwisho'.

2. Maana ya Maitreya ni 'Mrehemevu'. Mtume Muhammad anelezewa katika Qur'ani (21:107) kuwa ni '*mrehemevu*' kwa walimwengu wote.

3. Maitreya atakuwa na wasifu wote wa Buddha: Atatoka kwenye ukoo wenye heshima, atajitenga kwenye pango na kuzuriwa na Malaika, atakuwa na wake na watoto, atafanya kazi kuendesha maisha, na atakamilisha uhai wake kwa kawaida, yaani, atakufa kifo cha kawaida. Wasifu wote huu unamuelekea Mtume Muhammad.

4. Maitreya atakuwa mtawala. Muhammad hakuwa ni mtume tu bali alikuwa mtawala wa taifa la Kiislamu.

5. Maitreya atawazungumzia Mabuddha waliopita. Muhammad alizungumzia kwa wingi juu ya mitume iliyopita. Qur'ani inataja hadithi za watume ishirini na nne waliokuja kabla ya Mtume Muhammad.

6. Maitreya hatokua na mwalimu katika dunia. Mtume Muhammad hakuwa aliyesoma na hakuwa na mwalimu wa kidunia. Elimu yake yote ilikuwa kwa ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa ufupi, uhalisi wa Mtume umo katika tabia yake ya heshima, ujumbe aliokuja nao, mabadiliko ya kudumu katika ustaarabu wa mwanadamu uliotokana na harakati yake, na kutabiriwa kwake kwenye maandiko ya dini zote kubwa.

***Muhammad, Salaa na amani za Allah zimfikiye.***



# Historia na Ujumbe wa Qur'ani

Qur'ani ni maandiko yaliotoka kwa Allah alioteremshiwa Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) kupitia kwa Malaika Jibril. Qur'ani ni ufunuo wa mwisho kutoka kwa Allah kwa wanadamu wote mpaka mwisho wa dunia. Qur'ani imeteremshwa kuukamilisha ujumbe wa Allah kwa wanadamu, kuthibitisha yaliyoteremshwa kabla yake na kusahihisha mabadiliko yaliyo ingizwa ndani ya mabaki ya vitabu vilivyopita.[11]

## Kuteremshwa kwake

Qur'ani iliteremshwa kidogo kidogo kwa hatua, katika lugha ya Kiarabu, kwa muda wa miaka 23, kuanzia mwaka 610 mpaka 632 CE. Huku kuteremshiwa Qur'ani kidogo kidogo kuliwaletea waumini muongozo wa kupangilia kwa mujibu wa hali maalumu zinazotokezeya. Pia ilihakikisha kuwaingia watu sheria za Allah vizuri na kutekelezwa vizuri katika maisha ya waumini.

## Kusajiliwa na kuhifadhiwa kwake

Kila anapo pokea ufunuo, Mtume (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alikuwa akiwaamuru waandishi wake waandike yaliyoteremshwa, huku na yeye akishuhudia na kusimamia. Wakati huo huo, Mtume na wengi katika masahaba zake, wa kiume na wa kike, walidhihifadhi kwa moyo aya hizo kama zilivyoteremshwa. Kwa njia hii Qur'ani iliandikwa na kuhifadhiwa moyoni na waumini wa kiume na kike katika wakati wa uhai wa Mtume. Mazoezi ya kuhifadhi moyoni Qur'ani yanaendelea mpaka hivi leo. Wakati wowote ule katika historia ya Uislamu wapo mamilioni ya Waislamu ambao wamehifadhi Qur'ani nzima katika maandishi yake asili na halisi. Leo inakisiwa kuwepo zaidi ya Waislamu milioni ishirini ambao wamehifadhi Qur'ani kamili, na mamilioni wengine wamehifadhi sehemu kadha ya Qur'ani.

## Yaliyomo na dhamira yake

Qur'ani ina sura 114. Idadi ya aya zilizomo ndani ya sura inatafautiana, kuanzia aya 3 (Sura 103 na 108) mpaka aya 286 (Sura 2). Qur'ani ni kitabu

cha muongozo, onyo na mabashirio mema, na pia chenye maelezo ya umma zilizopita na watume wake. Kwa ujumla inagusia dhamiri nne:

**Kwanza:** Inatueleza kuhusu Allah; Jinsi yake na Sifa zake. Kwa mfano tumeona Sura 112 katika Mlango wa 2 wa kitabu hichi inavyoeleza Upekee wa Mungu (*Tawheed*) na sifa Zake za pekee ambazo hazina ushirika na mwengine yoyote. Aya ifuatoyo hapo chini, ijulikanayo kwa 'Aya ya Kiti cha Enzi' (kwa Kiarabu *Ayatul Kursi*) ni mfano mwengine unaoelezea sifa za Allah:




***Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu. (Qur'an 2:255)***

**Pili:** Inaelezea juu ya uhusiano baina yetu na Allah; kwa nini Alituumba na nini wajibu wetu Kwake. Kwa mfano, Allah anasema katika Qur'ani 51:56:

> ***Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.***

Katika aya hii, neno '*ibada*' linamaanisha kumtumikia Mwenyezi Mungu Muumba na kuishi kwa kufuata maamrisho Yake. Tena Qur'ani inaelezea juu ya uhusiano baina yetu na viumbe vyengine vilivyobakia; Malaika, Majini, ulimwengu wa wanyama na dunia yote; nini umuhimu na maingiliano yao kwenye uhai wetu.[12]

**Tatu:** Inatoa muongozo kwa kuweka sheria na kuonesha njia iliyosawa, na inaweka nguzo na kipimo cha tabia njema za maisha. Inaahidi pepo ya milele kwa wale wanaofuata muongozo huu na inaahidi mateso ya milele kwa wale wenye kwenda kinyume na muongozo huu.[13]

**Mwishowe,** Qur'ani inatuambia kuwa umma zote zilizopita zilipewa muongozo kupitia kwa mitume. Kwa mfano, katika 10:47 Allah anasema:

> ***Na kila umma una Mtume. Alipo wajia Mtume wao walihukumiwa baina yao kwa uadilifu, wala hawakudhulumiwa.***

Maalezo ya umma zilizopita ni kisomo kwa wanadamu juu ya matokeo ya vitendo vya umma hizo. Kwa mfano, Qur'ani inatuhadithia juu ya shida aliyopata Mtume Nuh kwa watu wake na mafuriko yaliyofuatia. Inatuhadithia juu ya shida aliyopata Mtume Musa kwa watu wake na kwa Firauni. Na tena kuna "bora ya hadithi zote", hadithi ya maisha ya Mtume Yusuf. Kwa ujumla, Qur'ani inaelezea hadithi za watume 25 kati ya maelfu ambao Allah aliwatuma kwa wanadamu katika zama zote.[14]



*Kusoma Qur'ani ni kitendo cha ibada katika Uislamu. Kwa sababu hii, leo Qur'ani ni kitabu kisomwacho zaidi kuliko kitabu chochote duniani.*

## Ulingano wa Qur'ani na sayansi ya kisasa.

Qur'ani iliteremshwa karne kumi na nne zilizopita. Juu ya hivyo, tunaona ndani yake mengi ya ilimu ya kisayansi ambayo utaalamu wa kisasa umeyavumbua katika nyakati za karibuni tu. Ilimu hii ya sayansi inagusia nyanda nyingi, katika hizo zikiwemo unajimu, jiolojia, fizikia, biolojia,

elimu ya wanyama na nyenginezo. Tutazame mifano michache.

## Kuumbwa kwa Ulimwengu

Katika Qur'ani (21:30), Allah anasema:

> ***Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibambatua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?***

Na katika Sura 51 aya 47 Allah anasema:

> ***Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio twenye uwezo wa kuzitanua.***

Aya hizi zipo sawa na ilimu ya kisasa ya kuwa ulimwengu ulianza kutokana na kitu kimoja (katika hali ya mvuke) ambacho kikaripuka na kuzalisha makundi ya nyota (galaxies). Tokeo hili linajulikana kwa jina la 'Big Bang' (Mripuko Mkubwa). Vilevile, elimu ya sayansi ya kisasa inathibitisha kuwa ulimwengu ungali unapanuka tangu tokeo la mripuko wa mwanzo.

## Kukua kwa mimba

Katika sehemu mbali mbali Qur'ani inaelezea hatua za kukua kwa mtoto ndani ya mimba, kwa mfano;

> ***Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. (Qur'an 23: 12–14).***

Aya hizi zinaelezea kwa uwazi kabisa na kwa usahihi kule kukua kwa mimba kuanzia pale inaposhika, tena kwa maneno sahihi ya Kiarabu. Kwanza, mbegu ya mimba hukua na kuchukua umbo la damu iliyogandamana (*'alaqah*), tena hukua katika umbo la kidonge (*mudghah*). Baada ya hapo mafupa yanaanza kukua ndani ya kidonge hicho na mwishowe nyama inaanza kukuwa juu ya mifupa. Hivi ndivyo Qur'ani inavyo elezea kukua kwa mtoto.

Maneno mawili ya Kiarabu yaliyotumika katika aya, *'alaqah* na *mudghah*, ni muhimu sana katika usahihi wake.

Mbali na kuwa na maana ya damu iliyogandamana, *'alaqah* pia ina maana ya 'kitu kilichojitundika' na ina maana ya 'kitu chenye mfano wa ruba'. Tukiangalia mimba katika hatua za mwanzo tutaona kuwa imejitundika kwenye kuta ya tumbo la uzazi, sio yenye kuelea tu. Pia ina umbo la mfano wa ruba. Ruba ni kidudu kinachoganda kwenye ngozi ya mnyama na kunyonya damu. Pia mimba katika hatuwa hii hupata damu kutoka kwa mama kupitia kondo (placenta).

*'alaqah* hukua na kuchukua umbo la *mudghah*, ambayo maana yake 'kidonge cha nyama kilichotafunwa'. Tukiangalia mimba katika hatua ya baada ya *'alaqah*, tutaona kuwa ina sura ya ubani uliotafunwa wenye alama za meno.

Haya ni maelezo wazi na ya kushangaza ya kukua kwa mimba ambayo yalitolewa kwenye Qur'ani katika karne ya 7. Wanasayansi wameweza kuthibitisha maumbo hayo baada ya uvumbuzi wa ala za darubini katika karne ya 19.

Jambo jengine la kuvutia lililotajwa katika Qur'ani ni kuwa mtoto katika tumbo la uzazi amekingwa (amezingiwa) na mapazia matatu ya giza. Katika aya 39:6 ya Qur'ani, Allah Anasema:

*Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu..*

Kwa ilimu ya kisasa tunajua kuwa mtoto katika tumbo amekingwa na; kwanza ukuta wa tumbo la mama, pili ukuta wa uterasi na tatu ngozi nyembamba ya 'amnio-chorionic'. Hizi ndio pazia tatu, uthibitisho mwengine wa usahihi wa taarifa za Qur'ani.






*Picha iliyo kushoto inaonyesha mimba katika hatua ya "mudghah" ambayo imefanana sana na ubani uliotafunwa. Picha ya kulia inaonyesha mimba katika tumbo inaning'inia katika ukuta wa tumbo na imekingwa na mapazia matatu.*

## Umuhimu wa Milima

Tunaiona mandhar ya milima ilivyotandaa kama mawimbi juu ya ardhi, yenye kupendeza na kuvutia. Lakini kwa uhakika, milima inatekeleza wajibu muhimu sana wa kuweka imara ardhi ya dunia. Sehemu iliyo chini ya gamba la juu la ardhi ni nyepesi na kama tope nzito, kwa hiyo, sehemu ya ardhi iliyo juu yake inahitaji kitu cha kuiweka imara. Wanasayansi

wamegundua kuwa kinachoiweka ardhi kuwa imara ni milima, ambayo ina mizizi chini ya ardhi. kwa hivyo milima inatumika kama vigingi.

Allah anasema katika Qur'ani (21:31):

> ***Na tukaweka katika ardhi milima iliyo thibiti ili (ardhi) isiwayumbishe.***

Na katika sura 78 aya ya 6 na 7, Allah anasema:

> ***Kwani hatukuifanya ardhi kama matandiko? Na milima kama vigingi?***

Aya hizi zinazoonesha kazi ya milima zinakubaliana kabisa na utaalamu wa sasa wa kisayansi. Fikra ya kuwa milima ina mizizi ilianzwa katika mwaka 1865 na maarifa ya kuwa mizizi hiyo ndio yenye kuimarisha ardhi ilikuzwa mwishoni mwa karne ya 20. [15]




***Mchoro uoneshao mlima na mzizi uliozama katika mantle ya dunia.***

## Maji ni asili ya Uhai

Inajulikana kikawaida kuwa maji ndio chanzo cha maisha, walakini, Qur'ani imekwenda mbele zaidi kwa kueleza kwa mkazo kuwa kwa hakika kila kiumbe chenye uhai kimetokana na maji. Kuongezea juu ya aya 21:30 iliyotajwa ukurasa wa 34, tunasoma katika aya 25:54;

> ***Naye (Allah) ndiye aliye muumba mwanaadamu kutokana na maji, akamjaalia nasaba (ya damu) na ujamaa wa ndoa. Na Mola wako Mlezi ni Muweza.***

Hivi sasa ni ukweli uliothibitika ya kwamba maji ni asili mia 80 (80%) ya chembe chenye uhai (cell), na kwamba viumbe vyote venye uhai vinayo maji kwa uchache, asili mia 50 (50%). Zaidi ya hayo, kama tujuavyo, viumbe vyote venye uhai vinahitaji maji.



***Maji ni Uhai: Kubadilika kwa majira ya hali ya hewa duniani na athari yake ya ukamwe wa mvua yanaangamiza maisha ya wanyama na mimea katika sehemu nyingi za dunia.***

Taarifa hizi za kitaalamu tulizozitaja ni mifano michache kati ya nyingi za taarifa za kisayansi zinazopatikana ndani ya Qur'ani ambazo ziliteremshwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita, wakati watu walikuwa na elimu ndogo sana ya unajimu, fizikia na baiolojia. Taarifa hizi zinakubaliana kamili na elimu ya sayansi ya kisasa, na mengi yaliotajwa ndani ya Qur'ani yamejulikana hivi karne iliyopita tu, kwa sababu ya maendeleo ya ilimu ya sayansi ya sasa.[16]

# Uhalisi wa Qur'ani

Jee, hali Qur'ani ni kweli ufunuo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu? Hili ni suala la halali, kwa sababu leo duniani kuna maandiko mengi, ambayo yanapingana katika yaliyomo, na bado kila moja inadai kuwa imetoka kwa Mungu. Kuongezea katika suala hili, baadhi ya watu wanaweza kuuliza: Tuna uhakika gani kuwa Qur'ani haikubadilishwa kupitia miaka yote hiyo iliyopita?

Majibu ya masuala haya yanapatikana katika Qur'ani yenyewe, ambayo imetoa vigezo vitatu (au hoja tatu) za kuufafanuwa ukweli.

## Kigezo cha kwanza

Ufunuo wa kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu umefungamana kwa ukamilifu, na hauna hitilafu yoyote ndani yake. Allah anasema katika Qur'ani 4:82:

> ***Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake hitilafu nyingi.***

Maandiko yoyote yenye hitilafu au kuwa na makosa ndani yake hayawezi kutokana na Mwenyezi Mungu. Qur'ani kamwe haina hitilafu wala utata. Hii pia inathibitisha kuwa haikubadilishwa na mikono ya mtu kupitia miaka yote. Hayo yaonekanayo kuwa yana hitilafu ambayo mara kwa mara hutajwa na wakosoaji yanatokana na ukosefu wa ujuzi sahihi wa lugha ya Qur'ani ya Kiarabu na mahusiano na hali ya kuteremshwa hizo aya zinazotajwa.

## Kigezo cha pili

Ufunuo wa kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu unapindukia uwezo wa mwanadamu katika kutimiza mahitajio ya mwanadamu kwa marefu na mapana; katika sheria, uadilifu, murua na muongozo wa kiroho, na

pia una nguvu za mijadala, hoja, ufasihi wa maneno na mtindo. Kwa hivi, Allah amempa mwanadamu changamoto ya kuleta kitabu japo cha kufanana na Qur'ani. Katika aya 2:23 – 24, Allah anawapa changamoto hao wasioamini:

> ***Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake, na muwaite mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli. Na msipofanya - na wala hamtofanya kamwe - basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe walio andaliwa hao wanao kanusha.***

Allah anaongezea changamoto hiyo katika aya 17:88:

> ***Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.***

Ni pekee Muumba Mwenye Ujuzi wa Yote anayeweza kutoa changamoto hii. Hakuna mtu awezae kuandika kitabu kisha akadai kuwa hakuna awezae kuandika kitabu kama hicho, sasa au katika mustakbal. Na zaidi, ikiwa Qur'ani imepata kubadilishwa na mtu, wangaliweza watu wengine kutoa kitabu chenye kufanana nacho. Changamoto hii imesimama mpaka leo kama ilivyo simama miaka 1400 iliyopita.

## Kigezo cha tatu

Ufunuo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu ni lazima uwe unafaa na kutimka wakati wote na ubakie wenye kukubaliana na ilimu ya mwanadamu kila inapoendelea, na mahitajio ya mwanadamu yanavyobadilika na kukua. Kanuni za Qur'ani katika sheria, haki, biashara, nidhamu ya jamii na tabia njema zinafaa na kutumika leo kama zilivyokuwa zaidi ya miaka 1400 iliyopita wakati Qur'ani ilipoteremshwa. Na zaidi ya hayo, kama ilivyoelezwa katika Mlango wa 6, Qur'an inakubaliana kamili na kila

pande za ilimu ya kisasa katika sayansi za maumbile.

Ingelikuwa Qur'ani imetokana na mtu, sio Mwenyezi Mungu, au ingelibadilishwa, basi kufaa na kutumika kwake leo kungelipotoka na kusingewezekana. Kwa milele Qur'ani itafaa na kutumika katika kila pande za ilimu ya mwanadamu na mahitajio yake.

Vigezo hivi, pamoja na mengine yaliyomo ndani ya Qur'ani, vyote vyenye athari nzito na nguvu za kutosheleza mahitajio ya mwanadamu na muongozo, vinadhihirisha na kuthibitisha muujiza wa Qur'ani. Kwa hakika Qur'ani ni muujiza pekee alioudai Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye), ijapokuwa kwa idhini ya Allah alifanya miujiza mingi katika ujumbe wake wa utume.





***Qur'ani Sura ya 7, aya 86-87 katika maandiko asili (kulia) na maandishi ya baadae (kushoto). Katika wakati wa Mtume, maandishi ya Kiarabu yalikuwa ni herufi bila ya kuonesha alama za matamko na usomaji. (kwa Kiarabu – tashkil na i'jam). Uislamu ulipoenea kwa watu wasiozungumza Kiarabu, makosa ya usomi na matamshi ya Qur'ani yalidhihiri. Kujiepusha na hatari hiyo, alama za matamko na usomaji zikaingizwa mnamo karibuni miaka sitini baada ya kufa kwa Mtume.***

# Dasturi na Mafundisho ya Mtume

Dasturi na mafundisho ya Mtume (kwa Kiarabu *Sunnah* au *Sunan*), ni mafundisho na mifano ya kimaisha ya Mtume yaliopokelewa na masahaba wa Mtume. Sunnah asili yake ni ufunuo (Qur'ani 53:3), lakini ni tafauti na Qur'ani. Sunnah ni msingi wa pili baada ya Qur'an wa mafundisho ya Uislamu.

Qur'ani iliteremshwa, ikahifadhiwa kwa maandishi na kukusanywa pamoja wakati wa uhai wa Mtume, lakini Sunnah zake sana zilihifadhiwa na kuwekwa pamoja baada ya kufa kwake (632 CE). Kuhifadhiwa kwa Sunnah kulianza punde baada ya kufa kwa Mtume, lakini kukusanywa pamoja kulianza hasa kati ya karne ya nane na kusitawi katika karne ya tisa. kwa mfano, *Musnad Ar-Rabi' bin Habib* ni mkusanyo uliokamilishwa mwishoni mwa karne ya nane, na *Sahih Al Bukhari* na *Sahih Muslim* zilikusanywa katika karne ya tisa.

Sunnah zilikuwa zikisimuliwa na kuendelezwa na watu wengi kupitia zama. Kwa hivyo ilibidi ziwepo njia za ufafanuzi za kuzithibitisha Sunnah. Njia hizo zilichambua mtungo wa wasimulizi, yaliyomo katika hadithi, munasaba na mazingira ya kunukuliwa hadithi yenyewe. Kupitia njia hii ya ufafanuzi, Sunnah (au hadithi) ziliwekwa katika mafungu kadha kufuatana na uthibitisho wake. Njia hii ya uthibitisho (inayoitwa *isnaad* kwa Kiarabu) inatumika hadi hivi sasa kubainisha hadithi za uongo ambazo zilipenya katika mkusanyo wa asili.

Sunnah za Mtume zinatumika katika mambo yafwatayo katika muongozo wa Kiislamu na utungaji wa sheria:

1. Zinabainisha dhamiri za aya za Qur'ani zilizoteremshwa, na kuzifafanua maana zake.

2. Ni shina la pili asili la sheria ya Kiislamu baada ya Qur'ani, na maamrisho yake kuhusu kipi kinachoruhusiwa na kipi kinachokatazwa, yanalazimika kama ni amri za Qur'ani.

3. Zinasimamisha amri ya Qur'an kwa kutiliya mkazo maamrisho ya Qur'ani.

4. Zinafafanua utaratibu wa kufanya ibada zilizoamrishwa ndani ya Qur'ani.

5. Zinaelezea na kuweka mifano juu ya utekelezaji wa tabia njema zilizomo ndani ya Qur'ani.

Ifuatayo ni mifano mitatu ya hadithi au sunnah za Mtume.

> ***Amesimulia Abu Ubayda kuwa Jaabir bin Zaid alisikia kutoka kwa Ibn Abbas (Radhi za Allah zimfikie) kuwa Mtume (Salaa na amani za Allah zimfikiye) amesema; "Yoyote yule anayelaghai sio miongoni mwetu, na yoyote yule asiokuwa na huruma kwa wadogo na asiokuwa na heshima kwa wazee sio miongoni mwetu". (Musnad Ar-Rabi' bin Habib, Hadithi No. 582)***

> ***Alisema Abu-Minhal, "Niliwauliza Al-Bara bin Azib na Zaid bin Arqam kuhusu kazi ya kubadilisha sarafu (money exchange). Wakajibu, "Tulikuwa ni wafanya biashara wakati wa Mtume wa Allah (Salaa na amani za Allah zimfikiye) na tukamuuliza juu ya kubadilishana sarafu". Akajibu, "Ikiwa ni mkono kwa mkono basi hakuna dhara ndani yake, kwa njia nyengine hairuhusiwi" (Sahih Al Bukhari, Kitabu cha Biashara, Hadithi no. 276)***

> ***Abu Hurairah alinukulia kuwa Mtume wa Allah (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alisema; Mwanamke asiozeshwe mpaka ashauriwe, na mwanamke bikira asiozeshwe mpaka itoke ruhusa kutoka kwake mwenyewe. Wakamuuliza Mtume, "Inapatikana vipi idhini yake (bikira)?" Akasema, "Kuwa amekaa kimya". (Sahih Muslim, Kitabu cha Ndoa, No. 008, No. 3303)***

Mifano hii ni miongoni mwa hadithi nyingi za Mtume ambazo zinafafanua sheria na kutoa muongozo katika maisha ya kijamii.

# Maisha baada ya Kifo

Kifo hakiepukiki na kwa hivyo mtu lazima apambane na yakini ya kuwepo uhai baada ya kifo. Anaweza mtu kuyakataa hayo kabisa, yaani, kujikinaisha moyoni kuwa hakuna kitu baada ya kufa, mwengine anaweza kuyapuuza hayo na kukaa na tamaa ya jema lolote lijalo, lakini kwa vyovyote vile mtu huyu anajitosa katika bahati nasibu ya hatari kwa sababu maisha baada ya kifo ni uhai wa milele, na hilo ni jambo zito mno. Jambo la busara ni kutarajia na kujiandaa na maisha baada ya kifo, na hii ndio lengo la dini; kujitayarisha kwetu kuyakabili maisha ya milele baada ya kifo, (yaani akhera).

**Uthibitisho wa kuwepo akhera**

Dini inatufundisha kuwa akhera ipo. Lakini pia yakini ya kuwepo uhai baada ya kufa inaweza kufahamika kwa hoja za kiakili na kwa mantiki. Zingatia hoja hizi zifuatazo:

**Hoja ya Mwanzo:** Miongoni mwa viumbe vya Mwenyezi Mungu, wanadamu wana akili, uwezo wa kuhoji na uhuru wa hiari. Sifa hizi zinatupa nguvu za uwezo za kiroho, kimwili na uvumbuzi kushinda viumbe vyote vyengine. Kwa sababu hiyo, alipoumbwa Adam Malaika waliamrishwa na Mwenyezi Mungu wamsujudie, kuutambua uwezo mkubwa aliopewa mwanadamu.[17] Na ndio vivyo, mwanadamu ametamba na uchunguzi wake wa ulimwengu, akaweza kuwasiliana dunia nzima papo kwa papo, kutoa vyakula vilivyogeuzwa kinasaba, wakavumbua vyombo venye uwezo wa kiakili, na mafinikio mengi ya maendeleo yanayokuja kwa vile elimu ya mwanadamu inavyopanuka. Haiwezekani kuwa hichi kiumbe kikubwa kinachoitwa **mwandamu** kuumbwa bila ya muumbaji kuwa na lengo au mpango wowote; tuishi na tufe tu – ndio yamekwisha? Hivi ndivyo watu wa zamani walivyojiamulia kama inavyotupasha Qur'ani**:**

> ***Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo***

***kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu. (45:24)***

Hakika fikra ya kuwa hakuna kitu baada ya kufa ni dhana za watu tu.

**Hoja ya Pili:** Kila kitu katika ulimwengu kinaonyesha ukamilifu wa hali ya juu wa ujuzi na usanifu wa Mwenyezi Mungu. Daima wanadamu wanaishi katika tamaa ya kupata maisha yenye kutosheleza zaidi katika dunia hii, maisha ya siha yenye kudumu na uhai wa daima; hakuna anayetaka kuumwa au kuwa na ufukara au kutaka kufa. Matamanio haya ya mwanadamu yana ashiria upungufu uliopo katika maisha ya kidunia. Kwa vile mwanadamu hawezi kutamani kitu kisichokuwepo, ukamilifu ambao mwanadamu anautaka ni lazima uwepo. Ukamilifu huu ambao wanadamu wanautamani, kwa hakika upo katika maisha ya akhera ambapo ukamilifu wa mwisho kabisa katika uumbaji wa Mungu utathibiti. Huku kuwepo kwetu duniani, mahala ambapo hapajakamilika, ni maisha ya kupita, ya kututayarisha na maisha yajayo ambayo ni kamilifu na ya milele, na huu ni mpango wa mungu katika kuumbwa kwetu.

**Hoja ya Tatu:** Wanadamu wameumbwa na uhuru wa kuchagua (hiari); Wengine tunaweza kuwa waongofu na wengine tunaweza kuchagua kuwa waovu na wabaya. Wabaya wanawatia katika maafa wanadamu wenzao na wakaweza kuepuka na sharia na hukumu kwa sababu mbali mbali; kwa mfano, nguvu ya cheo chao, udhaifu wa kanuni za kibinadamu, ufisadi katika nidhamu ya sheria, na kadhalika. Na wengine wanaweza kufanya uhalifu mkuba mno kiasi cha kwamba hakuna hukumu ya kibinadamu yenye kotesheleza malipo yake; zingatia mfano wa mtu aliyehusika na mauaji ya watu milioni; adhabu gani hasa inaweza kutosheleza hukumu ya mtu kama huyo? Hukumu ya juu kabisa, ya haki haiwezekani kamwe kutosheleza hapa duniani. Matamanio yetu ya kupata hukumu ya kweli yanaweza kutimizwa akhera tu. Kwa hakika itakuwa sio haki kabisa ingekuwa hakuna akhera.

**Hoja ya Nne:** Kama ilivyotajwa kabla, wanadamu wameumbwa na utambuzi wa asili wa ukweli wa huluku ya Mwenyezi Mungu na lengo lake (*Fitrah* kwa Kiarabu). Hivyo, tunaona kwamba katika historia yote ya mwanadamu, watu wengi mno wanaamini maisha ya baada ya kifo. Kwa mfano, rekodi za kihistoria za ustaarabu wa kale zinaonyesha kwamba wengi ya watu walijitayarisha kwa maisha baada ya kifo chao. Walitambua vyema kwamba kifo kinatupeleka kwenye uendelezi wa maisha ya roho katika maisha mepya na ulimwengu mpya.

**Hoja ya Tano:** Qur'ani inaelezea juu ya: (a) maajabu mbali mbali katika elimu ya maumbile (tazama Mlango wa 6), (b) matukio mbali mbali katika historia, (c) sheria na mifano ya utu mwema, ambayo yaliutengeneza ustaarabu wa mwanadamu na mpaka leo yanaendelea kuwa na athari kubwa juu ya mwanadamu. Hakuna moja katika maelezo haya ni ya uongo au yasiokubalika. Kwa ukweli huu uliothibiti wa Qur'ani na uhalali wake, kwa nini mtu ahoji uyakini wa kuwepo akhera, kitu ambacho Qur'ani kinazungumzia kwa mkazo sana?

Hoja tano hizi zinamtosheleza mtu yoyote ya kuwa uhai baada ya kifo sio tu yakini bali ni lazima uwepo. Juu ya hayo, kuna hoja yoyote inayo onesha kutokuwepo kwa akhera?

## Mafundisho ya Kiislamu kuhusu Kifo na Uhai Ujao

Roho ya mwanadamu inapitia awamu mbalimbali katika uhai wake wa milele. Maisha yetu hapa duniani ni matayarisho ya awamu zifuatazo za uhai. Kifo ndio chanzo cha awamu ifuatayo ya uhai wetu, nayo ni 'awamu ya katikati baina ya kufa na kufufuliwa'. Awamu hii kwa Kiarabu inaitwa Barzakh. Huu ni muda upitao ndani ya kaburi ambamo mtu huamka katika upande mwengine wa uhai akiwa na fahamu kamili ya kiroho. Wale waliojitayarisha na akhera katika maisha haya ya dunia wataingiwa na furaha na kutua (nyoyo zao) kwa sababu ya hisia na matarijio ya raha na ya kutosheleza huko mbele wendapo; ambapo wale

waliopuuza uyakini wa akhera watakuwa na majuto makubwa kwa vile yanavyokaribia maafa yanayowangojea. Qur'ani inatuarifu kuwa wakati wa kufariki, roho inajulishwa na Malaika hali gani katika hali hizo mbili inayomkabili:

> ***Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakenda mwendo mzuri, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa. (Qur'an 41:30)***

> ***Na laiti ungeli ona Malaika wanapo wafisha wale walio kufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao, na kuwaambia: Ionjeni adhabu ya Moto! (Qur'an 8:50)***

Kipindi hichi cha kaburini ni hatua ya mwanzo ya kuelekea akhera ambacho kinatuashiria matukio ya yale tuliyoyachagua katika uhai wa duniani. Inasemekana kuwa Mtume alisema; "Kaburi ni hatua ya mwanzo ya uhai ujao. Atayepitia hapo kwa salama, basi yanayofuata ni mepesi kuliko hapo. Lakini asiyefanikiwa katika hatua hiyo, basi yafuatayo kwake ni makali zaidi kuliko hapo."

Roho inabakia katika hii hali ya kati kati mpaka Mwisho wa Zama au Saa itapofika, wakati ambapo dunia hii tuijuayo itageuzwa iwe katika umbo jengine kabisa la uhai. Utakuwa Ulimwengu Mpya. Hili ni tukio kuu mno ambalo limeelezewa katika Qur'ani kwa uwazi kabisa. Mfano, tunasoma katika aya ya 22:1-2;

> ***Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu. Siku mtapoiona kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake. Na utaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa, lakini ni adhabu kali ya Mwenyezi Mungu (inayowafanya wayumbeyumbe kama wamelewa).***

Mwisho wa Zama unaashiria kuja kwa Ulimwengu mpya ambao utaanza kwa kufufuliwa wafu; wanadamu wote wataumbwa tena. Qur'ani inaielezeya siku hii kuwa ni siku ngumu sana, hasa kwa wale wasiokuwa wakiamini ambao watalilia kupewa fursa nyengine ya maisha ya duniani ili wayatengeneze waliyotenda. Ama kwa waumini, hawatokuwa na khofu siku hiyo.[18]

Wanadamu watakusanywa ili wahukumiwe. Hii ndio Siku ya Hukumu ambayo ni nzito mno, hata Qur'ani kuitaja kwa majina mengi; Siku ya Majuto (19:39), Siku ya Ushindi (32:29), Siku ya Maafa Makuu (76:10), Siku Nzito (76:27), Siku Kubwa Mno (19:37), Siku ya Hisabu (38:16, 40:27), na kadhalika. Siku ya Hukumu ni siku ambayo thamani ya nafsi zetu itadhihirishwa na Mola wetu. Itakuwa ni siku ya raha kubwa na matarijio ya furaha kwa wale walioongoka, na itakuwa siku ya majuto na malalamiko kwa waliokuwa wakimkanusha Mwenyezi Mungu na Siku hii ya Hukumu. Aya za Qur'an zifwatazo zinatupa picha ya hali hizi mbili:

> ***Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako Mlezi, basi utamkuta. Ama atakaye pewa daftari lake kwa mkono wa kulia, basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi, na arudi kwa ahali yake kwa furaha. Na ama atakaye pewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, basi huyo ataomba kuteketea. Na ataingia Motoni. Hakika alikuwa furahani kati ya jamaa zake. Huyo hakika alidhani kuwa hatarejea tena kwetu. (84:6-14)***

Uislamu unatufundisha kwamba katika akhera waja wema watakutanishwa na waja wema miongoni mwa familia zao na wawapendao;[19] Ni raha iliyoje kukutana peponi na wazee wetu, kaka zetu na dada zetu, watoto wetu, na rafiki zetu. Lakini kwa wale waovu, itakuwa mandhari isiyotamanika kabisa kabisa; watatamani kuwe wasingekuwapo (wasingeumbwa):

> ***Hakika tumekuhadharisheni adhabu iliyo karibu kufika; Siku ambayo mtu atakapo ona yaliyo tangulizwa na mikono yake; na kafiri atasema: Laiti ningeli kuwa udongo! (Qur'ani 78:40)***

# Mtizamo wa Kiislamu juu ya Dini nyengine

Wanadamu wameumbwa na asili ya kumtambua Muumbaji na tabia njema za utu (Kwa Kiarabu *Fitrah*). Kupitia historia yote ya wanadamu Mwenyezi Mungu aliwatuma mitume kwa mtungo kwa kila umma kuiamsha hii asili ya kawaida iliyomo ndani ya wanadamu. Ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watume wote ulikuwa daima wenye mfumo mmoja wa msingi wa imani – Upekee wa Mungu, Kuamini Akhera na Uongofu – ijapokuwa sheria na aina za ibada zilikuwa na tafauti[20]. Allah anasema katika Qur'ani 42:13;

> ***Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe (Muhammad), na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Issa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni magumu kwa washirikina hayo unayo waitia. Mwenyezi Mungu humteua kwake amtakaye, na humwongoa kwake aelekeaye.***

Kufarikiana katika kanuni za imani na dini kumekuja baada ya zama kupita kutokana na kupotoka kidogo kodogo kutoka kwenye ujumbe asili. Katika Qur'ani Allah anawaita wanadamu kurudi kwenye imani ya msingi aliyoitekeleza Ibrahim ambaye alikuwa mkweli katika imani yake ya Mungu Moja, na ni mzee wa mitume wa Mwenyezi Mungu waliokuja baada yake katika historia ya wanadamu. Kwa hiyo, kwa mtizamo wa Kiislamu dini zote ziliokuwepo zinaingiya katika makundi mawili.

## 1. Dini za Imani ya Mungu Mmoja

Uyahudi, Ukristo na Uislamu ni dini ambazo zinashiriki katika mila moja za imani ya Mungu mmoja aliyokuja nayo Mtume Ibrahim (salama na baraka za Allah zimfikie). Katika asili, zote dini hizi tatu zina msingi mmoja wa kanuni za imani na dini.

Wayahudi na Wakristo wanaitwa "*Watu wa Kitabu*" katika aya nyingi

za Qur'ani.[21] Hii inamaanisha kuwa wao ni watu ambao wamehusikana na vitabu vya Mungu, nayo ni Taurati na Injili. Lakini, maandiko hayo mawili tuliokuwa nayo hivi sasa hayana mfumo wa kweli wa ujumbe asili wa watume waliokuja nao, Musa na Issa (salama na baraka za Allah ziwafikie)[22]. Kwa hivyo, Uislamu unaangalia Uyahudi na Ukristo kuwa ni dini ambazo haziambatani na mafundisho asili ya kweli ya Musa na Issa (salama na baraka za Allah ziwafikie).

Qur'ani iliteremshwa sio tu kuthibitisha na kukamilisha ujumbe wa Musa na Issa, bali pia kusahihisha upotofu uliomo katika yaliyobakia katika ujumbe wao.[23] Kwa sababu hii ndio mtizamo wa Kiislamu unaona kuwa wafuasi kweli wa ujumbe wa Musa na Issa kwa hakika ni wale wanaoifuata Qur'ani.

## 2. Dini Nyenginezo

Kuhusu dini zisizokuwa hizi mbili – Uyahudi na Ukristo, mfano, Uhindus, Ubuda na nyenginezo, Uislamu unaziangalia kama ni dini zilizo mbali kabisa na mila ya ujumbe wa mitume, na kwa hivyo hasihusiani na mila za Ibrahim. Baadhi ya dini hizo zimeelemea kwenye ukanaji Mungu, na nyengine zimepotea kabisa kutoka kwenye ibada ya Mungu Mmoja wa Kweli, Allah, kwa kumshirikisha Naye waungu wengine. Kushirikisha waungu wengine na Mungu wa Kweli Mmoja na Pekee ni kinyume na kanuni ya Upekee wa Mungu, (tazama Mlango wa 3).

Lakini, juu ya kuwepo tafauti zote hizi, Uislamu unaziheshimu imani zote pamoja na watu wanaozifuata imani hizo, kwa vile Allah Ndiye Aliyemuumba mwanadamu na akampa uhuru wa kuchagua katika itikadi za imani. Anasema katika Qur'ani 10:99;

> ***Angeli taka Mola wako Mlezi wangeli amini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?***

Haya yanasemwa tena katika aya 2:256:

> ***Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.***

Kwa hiyo, hitilafu katika imani ni katika mpango wa Allah katika kuumba wanadamu[24]. Kwa kutambua hilo, Waislamu kupitia historia wamekuwa wakiishi pamoja na watu wenye imani nyengine kwa usalama, mapenzi, ukarimu na maelewano. Ni muhimu kukumbuka kuwa Uislamu unailinda heshima ya mwanadamu na inatekeleza utu wema kufuatana na msingi wa kanuni ya usawa wa wanadamu na uhuru katika mambo ya imani.



***Hija ya kila mwaka huko Makka inawavuta zaidi ya watu milioni tatu wa mataifa yote kuja mahala pamoja kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Allah. Haji inadhihirisha na kuimarisha umoja wa dini na umoja wa wanadamu.***

# Yesu katika Uislamu

Moja katika nguzo za imani katika Uislamu ni kuamini Mitume yote ya Allah. Waislamu wanaamini kuwa Issa (au Yesu, salama na baraka za Allah zimfikie) alikuwa mmoja katika Watume wakubwa wa Allah.

Maisha na mafundisho ya Issa kama yaonekanavyo katika Biblia yaliandikwa miaka mingi baada ya kuondoka kwake na kwa hivyo mengi katika maandishi haya hayana uhakika. Qur'ani, ambayo inamtaja Issa mara ishirini na tano kwa jina lake, imekuja kuyaweka wazi yale yaliyobabaishwa na yale ya itikadi potofu juu yake Issa na mafunzo yake, kumuokoa yeye na mama yake kutokana na uzushi waliotupiwa nao, na kuwapa yeye na mama yake heshima ya kuwa ni waja wachamungu wa kweli wa Allah, radhi za Allah ziwafikie. Kwa hiyo, Qur'ani inatufundisha kuwa:

- Issa (salama na baraka za Allah zimfikie) alizaliwa baada ya mama yake Bikra Mariam kushika mimba ya kimuujiza. Kuambatana na hayo, hakuwa na baba na kwa hiyo hakuwa na ukoo wa upande wa baba, lakini alikuwa nao ukoo mtukufu kwa upande wa mama, kwa sababu Mariam ametokana na kizazi cha mitume. Lakini, juu ya mimba hii ya kimuujiza, Issa ni mwanadamu kamili, na kama Qur'ani inavyotuarifu, hakupatapo kudai kuwa yeye ni kitu zaidi isipokuwa ni mtu aliyechaguliwa na Allah kuwa ni mtume[25]. Kwa mfano, katika Qur'ani 5:116-117, Allah anaielezea mandhari moja ya Siku ya Hukumu:

  ***Na pale Mwenyezi Mungu atakapo sema: Ewe Issa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Issa) atasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka umekwisha***

***yajua. Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika Wewe ndiye Mjuzi mkubwa wa yaliyo fichikana. Sikuwaambia lolote ila uliyo niamrisha, nayo ni: Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipo kuwa nao. Na ulipo nifisha ukawa Wewe ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu.***

Kuna ushahidi mkubwa katika Biblia yenyewe kuwa Issa (salama na baraka za Allah zimfikie) alikuwa mnyenyekevu, alisisitiza hali ya utumwa wake kwa Mwenyezi Mungu, na kamwe hakudai uungu.[26]

- Alikuwa ni Masihi (Christ), maana yake kuwa alichaguliwa na Allah awe mtume.[27]
- Alifanya miujiza mingi, lakini kwa idhini ya Allah. Muujiza wa mwanzo ni wa kuwa alisema akiwa mtoto mchanga katika kumtetea mama yake, Mariam, ambae alikabiliwa na shutumu za uchafu kwa sababu ya kuzaa akiwa ni bikira. Baadae maishani mwake alifanya miujiza mingi mengine, kwa idhini ya Allah, kama vile kufufua wafu na kuponyesha vipofu (wakaona) na wenye ukoma.[28]
- Aliletewa Injili[29]. Kwa mfano, Katika Qur'ani 5:46 Allah anasema:

  ***Na tukawafuatishia hao Issa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na tukampa Injili iliyomo ndani yake uwongofu, na nuru na inayo sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Taurati, na uwongofu na mawaidha kwa wachamungu.***

- Alitumwa kwa watoto wa Israel tu (Wayahudi), sio kwa umma wowote mwengine. Allah anasema katika Qur'ani 3:49,

### *"Na ni Mtume kwa Wana wa Israili..."*

Hakika ya kuwa Issa (salama na baraka za Allah zimfikie) alitumwa kwa watoto wa Israel tu inaonekana hata katika Biblia za sasa, kwenye matoleo yake yote tafauti.[30]

- Hakuuliwa wala hakusulubiwa. Allah anasema katika Qur'ani 4:157–158:

> ***Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Issa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini, bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima. Wise.***

Kulikuwa na jaribio la maadui zake kutaka kumsulubu Issa (salama na baraka za Allah zimfikie), lakini Allah hakuwachia mtume Wake afedheheke: Alimlinda na kumuokoa mtume Wake.



***Msikiti wa Al-Aqsa uliopo Jerusalem, msikiti mtukufu wa tatu kwa Waislamu. Kama ilivyotajwa katika Qur'ani (17:1 & 53:13-18), Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alipanda mbinguni kutokea msikiti huu katika mwaka 621 CE.***

# Kwanini Uislamu, kwani dini zote si sahihi?

Kuna imani potofu ya kuwa dini yenye kufundisha ukarimu, usawa na mapenzi baina ya watu basi huwa yenye kukuelekeza kwa Mwenyezi Mungu na uchamungu, na kwa hiyo dini yoyote kama hiyo inakubalika. Kwa kauli nyengine, dini zote ni nzuri na/au sawa, kwa hivyo hahitajiki mtu kufuata dini maalumu. Muelekeo na fikra hizi zina makosa na kasoro kwa sababu mbili muhimu.

**Kwanza,** asili ya dini ni kule kumuabudu Mwenyezi Mungu Muumba Allah, mahusiyano baina ya sisi na Yeye, vipi tunamuabudu na vipi tunaendesha maisha yetu duniani kwa kufuata vile Atakavyo. Shuruti zote hizi lazima zitoke kwa Mwenyezi Mungu Muumba. Kwa hiyo, dini ya kweli na sahihi ni lazima iwe ile aliyoileta Mwenyezi Mungu Muumba mwenyewe.

**Pili,** haiwezekani kuwa sahihi kusema kuwa dini zote zilizopo leo ni za kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu Muumba, kwa sababu katika dini mbali mbali zilizopo leo kuna tafauti kubwa katika mafundisho na matendo yake. Kwa mfano; Sio dini zote kama wanavyo amini wafuasi wake zinakubaliana na imani ya Upekee wa Muumbaji, pili kuna tafauti kubwa baina ya dini mbali mbali kuhusu uokozi, na tatu, kuna tafauti baina ya dini mbali mbali juu ya nini kilicho halali na nini kilicho haramu.

Hakika Mwenyezi Mungu Muumba sio mwenye kuleta dini zenye kuhitalifiana. Kwa hivyo dini Yake lazima iwe sawa na ya thabiti kwa wanadamu wote – sawa na thabiti katika misingi ya imani na kanuni za matendo. Ni jukumu la mtu binafsi kuutafuta ukweli kwa elimu na mantiki. Asijidanganye mtu kuwa dini zote zina mazuri na kwa hivyo zinakubalika kwa Mwenyezi Mungu Muumba; dini pekee inayokubalika Kwake ni dini **Yake** tu.

Uislamu haudai uasili katika dini; ni dini ile ile iliyotangaziwa kwa vizazi vyote vya mwanzoni vya mwanadamu. Kule kufarikiana kwa dini katika

historia ya mwanadamu kulizuka kutokana na kwenda mbali na ujumbe asili wa mitume. Mjumbe wa mwisho, Muhammad, na ujumbe wa mwisho, hii Qur'ani, pamoja vimekuja kuwaongoza wanadamu kuelekea kwenye ujumbe asili. Kwa hiyo dini pekee inayokubalika kwa Mwenyezi Mungu ni ile inayofuatana na ujumbe huu wa mwisho – Islam, yenye maana ya kujisalimisha kwa Ayatakayo Yeye. Kwa hiyo Allah anasema katika Qur'ani 3:85,

> ***Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika walio khasirika.***

Uislamu ulikuwa ni dini ya watume wote wa Mwenyezi Mungu ambao walimtangulia mtume wa mwisho, Muhammad, katika hao wakiwemo Ibrahim, Musa na Issa (salama na baraka za Allah ziwafikie wote), kwa sababu wote walikuwa watiifu kwa Mwenyezi Mungu Muumba na walijisalimisha kamili katika amri Yake. Pia Uislamu ulikuwa ni dini ya wafuasi wa kikweli wa watume waliotangulia, ambao walishikamana na mafundisho ya kweli ya watume wao.



Idadi ya Waislamu duniani (%)



# Hadhari kwa Ukanaji Mungu na Kushuku kuwepo kwa Mungu

Ukanaji Mungu ni kukataa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, na hii pia inamaanisha kukataa kuwepo kwa akhera. Kushuku Mungu ni kutilia shaka kule kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Wote wawili, wakanaji na wanao shuku, wameweka msingi wao wa kukataa au kuwa na shaka kwenye sababu mbali mbali. Katika zama za kale sababu zilikuwa juu ya kutoweza kumuona au kuhisi kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, au juu ya maafa yanayomkuta mwanadamu; ikiwa kuna Mungu kwa nini tunapata maafa? Katika zama za sasa sababu zimekuwa za hali ya juu zaidi; kwa nini kuwepo kwa Mungu hakuwezi kuthibitishwa kisayansi? Pia, kwa vile tunaweza kuelezea kisayansi matukio mengi katika ulimwengu, hakuna msingi wa kuwepo kwa Mungu.

Uislamu unapambana na ukanaji au kushuku kuwepo kwa Mungu kwa kuinasihi nafsi ya mwanadamu kwa njiya ya akili na mantiki kutambua kuwepo kwa Mungu. Mwanadamu hana uwezo wa kumuona Mwenyezi Mungu kwa sababu kuna tafauti isio na kikomo baina ya Mwenyezi Mungu Muumba na umbile la alivyo viumba. Na zaidi ya hayo, ikiwa Mungu ana umbo la kiwiliwili tuwezacho kukiona, basi atakuwa amedhibitiwa na kuwemo ndani ya mipaka ya kawaida ya mahala, wakati na umbo. Hii ni dhana ya kipuuzi kabisa, kwa sababu mahala, wakati na umbo ni vitu vilivyoumbwa na kwa hivyo haiwezekani kuwa vimuwekee mipaka Muumbaji. Badili yake, Qur'ani inawaelekeza watu kwenye masuala ya kiakili kuhusu ulimwengu ili waweze kumtambuwa Mungu kwa kuangalia alivyoviumba. Katika Qur'ani, dalili za kuwepo kwa Mungu zinaitwa "ishara", (kwa Kiarabu *ayah*) ambazo zimo kwa mamia ndani ya Qur'ani. Katika sura 41, aya 53 Allah anasema:

> ***Tutawaonyesha ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi***

> ***kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?***

Kwa ahadi hii Qur'ani inamuelekeza mwanadamu kuzingatia juu ya dalili nyingi za kuwepo kwa Mungu kwa kuangalia ulimwengu aliouumba. Kwa mfano, katika Qur'ani aya ya 3:190, Allah anasema;

> ***Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko ishara kwa wenye akili.***

Naam, wanasayansi wamegundua hakika za kushangaza katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi; Kwa mfano (a) ulimwengu ulikuwa na chanzo, yaani ulianza pasipo na kitu chochote, (b) ulimwengu uliendelea kukuwa kwa kufuata kanuni na njia za kifizia sahihi na zilizofungamana (c) kuna sababu zaidi ya 200 zenye kuhusika na uwezekano wa maisha katika dunia, kwa mfano, umbali baina ya dunia na jua, mvuto wa ardhi, muundo wa hewa katika anga ya dunia, kuwepo maji na mengineyo.

Katika aya nyengine Allah anasema;

> ***Yeye ndiye anaye kuteremshieni maji kutoka mbinguni. Katika hayo nyinyi mnapata ya kunywa, na miti ya kulishia. Kwa hayo Yeye anaizalisha kwa ajili yenu mimea, na mizaituni, na mitende, na mizabibu, na kila namna ya matunda. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanao fikiri. (Qur'an 16:10-11)***

Katika aya hii zinatajwa ishara nyingi juu ya kuwepo kwa Mungu. Na tuchukue nukta moja tu katika hiyo aya, kufanyika kwa mvua: kunaingia ndani yake mamia ya kanuni za kifizia na vipimo madhubuti katika kusababisha uvukizi wa maji kutoka ardhini, kupanda kwa unyevu mbinguni, kugeuka kwa unyevu kuwa matone ya maji, kujikusanya kwa matone na kuwa mawingu, kutembea kwa mawingu yaliyobeba maelfu ya tani za maji, na kumwagika kwa matone na kunyesha mvua. Mafanyiko

yote haya (ya kuifanya mvua) yanaendeshwa na kanuni madhubuti za kifizia na vipimo madhubuti. Qur'ani inatuelekeza kuzingatia juu ya maelfu ya ishara hizi katika vilivyo umbwa. Kwa mwandamu mwenye mazingatio na kusikiya hoja, yote hayo yanamuashiria juu ya Msanifu Mkuu na Muumba, Mwenyezi Mungu. Sio jambo la mantiki kuchukulia kuwa usanifu wote huu wa kiakili, ugumu wake na usahihi wake katika kuumba ni tokeo la sudfa au bahati. Hakika wanasayansi wengi wa kisasa wamekubali hoja hizi za kimantiki kuwa Mungu yupo.[31]

Qur'ani pia inatuarifu kwamba wanadamu wameumbwa na asili ya kimaumbile ya kumtambua Mwenyezi Mungu Muumba na kujisalimisha Kwake, (kwa Kiarabu inaitwa *fitrah*).[32] Ushahidi wa haya ni kuwa tunapokutwa na maafa makubwa na kufahamu moyoni kuwa hakuna mwanadamu anayeweza kutusaidia, tunaelekea kwa Mwenyezi Mungu kupata msaada. Muumba wetu ametuletea watume na vitabu ili kuiamsha hii fahamu asili ya kumtambua Yeye. Lakini, kwa sababu Mwenyezi Mungu ametupa uhuru wa kuchaguwa, tuna uwezo wa kuikandamiza tabia ya kimaumbile ya kumtambua Yeye. Lakini Mwenyezi Mungu anatuambia katika Qur'ani kuwa wenye kuitika na mwito wa kumuamini Yeye, basi atawaongoza, na wale waliochagua kuuziba moyo wao na wasimuamini Mungu, basi atawaachia kupotoka, na huu ndio mpango wa Mwenyezi Mungu katika maumbaji Yake.[33]

Qur'ani yenyewe, ambayo ni ufunuo wa mwisho kuteremshiwa mwanadamu, ni ishara ya kuwepo kwa Mungu. Katika sura 4 aya 82 tunasoma;

> ***Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.***

Ukiichunguza Qur'ani kwa uwazi wa akili bila mapenedeleo, utaona wazi kuwa haiwezakani kuwa imeandikwa na mtu, (tazama Mlango wa 7).

Qur'ani ni ushahidi mkubwa wa kuwepo Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu ametuumba kwa lengo takatifu la milele na akatupa neema zaidi ya aliyowapa viumbe vyengine.[34] Maisha yetu hapa duniani ni ya kupita na makusudio yake ni kututayarisha na makao ya milele ya Akhera. Katika matayarisho haya imani yetu kwa Mwenyezi Mungu Muumba itapewa mitihani kupitia raha au kupitia mashaka. Na zaidi ya hayo, tutapewa mtihani kwa vile tunavyoutumia uhuru wetu wa kuchagua, na katika mtihani huu wa uhuru wetu wa kuchagua ndio maovu na mema yataingia kati ya maisha yetu; Mtu ndiye mwenye kuchaguwa na kuleta uovu na sio Mwenyezi Mungu. Tukitizama upande mwengine, mashaka na tabu si mtihani tu wa imani yetu, bali ni onyo juu ya vitendo vyetu. Na vilevile mara nyingi huwa ni katika shida ndio nyoyo zetu huamka na kupata mawazo yenye kujenga na kutafuta lengo la juu la maisha.



***Kupatwa kwa Jua: Tukio hili la kustaajabisha lisingaliweza kuonekana ila kwa sababu ya kuwa umbali wa Jua na dunia ni mara mia nne kuliko umbali wa Mwezi na dunia, na pia ukubwa wa Jua ni mara mia nne kuliko ukubwa wa Mwezi. Vipimo vya usahihi kama hivi vinaashiria kwa msanifu aliyesanifu mandhari hii ya kupendeza, Mwenyezi Mungu Muumba.***

# Hadhi ya Wanawake katika Uislamu

Uislamu umewaweka wanaume na wanawake kuwa wote ni wanadamu sawa mbele ya Mwenyezi Mungu Muumba. Wanaume na wanawake wanatafautiana kimwili, na kwa sababu hiyo wajibu wao katika familia na jamii unatafautiana, lakini wakati huohuo wajibu huo unategemeana; hakuna aliye mbora kushinda mwenzake. Aya ya Qur'ani (4:1) ifuatayo inaelezeya msimamo huu vizuri:

> ***Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana (haki zenu), na (tizameni) kizazi (wazee na jamaa zenu). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.***

Kinachoisema aya hii ni kuwa wanawake wana asili ileile ya wanaume, wote wana haki zao baina yao, na Allah anataka uwepo utu na heshima maalum kwa wanawake, hasa kwa mama.




Kwa kutekeleza mafundisho haya matukufu, Uislamu uliwatoa wanawake kutoka hali yao kuwa ni vifanya kazi vya wanaume, mila ya kiovu ambayo ilitamba duniani wakati ulipokuja Uislamu katika karne ya 7, na kuwanyanyua kuwa sawa na wanaume katika hali ya kiroho, kijamii na uchumi.[35] Kwa hayo, wanawake katika Uislamu wana haki ya kumiliki, haki ya urithi, haki ya elimu, haki ya kujiendeshea wenyewe maisha na haki zote walizo nazo wanaume.

Ukosefu wa haki unaowafika wanawake katika baadhi ya jamii za Kiislamu hautokani na mafundisho ya Kiislamu, bali hakika ni matendo ya kitamduni ambayo Uislamu umekuja kuyapiga vita. Kwa mfano, ndoa za kulazimishwa, au kuwanyima elimu wanawake, yote hayo yanatendwa katika baadhi ya jamii za Waislamu, likini ni haramu katika sheria ya Kiislamu.

# Msimamo Mkali wa Kidini na Vurugu

Msimamo mkali wa kidini na vurugu ni mambo yaliomo katika dini zote ulimwenguni, na kuwepo kwayo ni kukongwe kama dini zenyewe zilivyo. Katika dini zote lazima kutakuwepo baadhi ya watu wataokuwa na msimamo mkali na mawazo potofu katika imani yao. Vita vingi vinapiganwa na maovu mengi yanatendwa na watu kama hao kwa sababu ya msimamo wao huo mkali wa mawazo ya kidini. Ili kuuvunja mwelekeo huu wa mwanadamu, imani katika Uislamu inashurutisha itikadi ya uhuru wa dini na kuheshimu dini zote, kuhifadhi heshima ya mwanadamu, utukufu wa roho ya binadamu, haki na usawa kwa wanadamu wote.

## Uhuru wa Kuchagua na Heshima kwa Dini zote

Allah amemuumba mwanadamu na uhuru wa akili na kuamuwa katika mambo ya imani, na kwa hiyo imani katika dini yoyote haiwezi kulazimishwa kwa yoyote. Kuongezea juu ya aya 2:256 na 10:99 za Qur'ani zilizokwisha tajwa kabla (tazama Mlango wa 10), Allah anasema katika aya 11:118-119,

> ***Na Mola wako Mlezi angeli penda ange wafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana, isipo kuwa wale ambao Mola wako Mlezi amewarehemu; na kwa hiyo (kuwa na uhuru wa kuchaguwa) ndio Mwenyezi Mungu amewaumba.***

Hitilafu katika imani ni katika mpango wa Mwenyezi Mungu katika kutuumba, na hii inamaanisha kuishi pamoja na ustahmilivu baina ya watu wa imani zote.

## Utukufu wa Roho ya binadamu

Uislamu unakemea mauaji ya wasio na makosa na inakemea kitendo chochote cha kinguvu au kisicho haki kufanyiwa asie na makosa. Kuua mtu bila ya haki ni dhambi kubwa mno katika Uislamu. Allah Anasema:

> ***Aliye muuwa mtu ambaye hana makosa ya uwaji au uchafuzi***

> ***katika nchi, basi ni kama amewauwa wanadamu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa wanadamu wote. (Qur'an 5:32).***

Katika Uislamu, vita vinaruhusiwa katika kujilinda tu na katika kupambana na kila aina ya uchokozi na uonevu.[36] Lakini, vita vya haki kama hivyo hupiganwa na wale waliofanya uchokozi na uonevu, sio watu wasio na makosa na/au mali zao. Zaidi ya hayo, wito wa vita unatakiwa ufanywe na serikali ya haki (inayotawala) sio watu binafsi au vikundi. Katika Uislamu vita vinaendeshwa na sheria kali za upiganaji na vipi kuwatendeya mateka, watu wasio na makosa na pia mali zao.[37]

## Haki na Uadilifu

Kutokuwepo haki na uadilifu kunaleta itikadi za msimamo mkali na ya vurugu. Uislamu unaamrisha haki na uadilifu kwa watu wote, wawe na imani yoyote ile. Allah anasema katika Qur'ani, aya 60:8,

> ***Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.***

Kwa mafundisho haya, msimamo mkali na vurugu hayatokei katika Uislamu isipokuwa kwa sababu ya kutoyajua mafundisho ya Kiislamu, kuwa na msimamo mkali katika dini kupita kiasi, au kuendeshwa na mengine yasiyokuwa ya dini. Vurugu tulionalo leo duniani hasa zinatokana na malengo ya kisiasa, na hayana uhusiano wowote na dini au madhehebu katika dini, ijapokuwa jina la dini ndio linalotumiwa kuyafunika makusudio yake ili kupata ufuasi wa watu. Asili hasa ya mapigano na vurugu tanayoyaona ni mapigano ya nguvu za kutaka utawala, kupigania mali, utajiri, tamaa, kulipiana kisasi na matokeo ya uingilizi wa kijeshi wa kigeni. Uislamu ni maasumu kwa vita na aina nyengine za vurugu ambavyo vinaendelea kufanyika ulimwenguni kwa jina la dini.

# Jihadi katika Uislamu

Neno '*Jihad* ' ni la Kiarabu lenye maana ya 'kujitahidi kwa bidii' ili kufikia lengo fulani. Katika Uislamu neno hili linamaanisha 'kujitahidi kwa bidii katika kumtii na kumtumikiya Allah'. Aya nyingi katika Qur'ani zinawataka waumini kujitahidi kwa bidii kwa ajili ya Allah. Kwa mfano, katika aya 5:35 tunasoma:

> ***Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia. Na hangaikeni kwa juhudi kwa ajili Yake ili mpate kuokoka.***

Kwa hivyo, kila kitendo cha muumini ambacho kimefanywa kwa nia ya kumtii Allah na kupata radhi zake ni *Jihad*; miongoni mwa vitendo hivyo ni ibada, utoaji sadaka, kujizuwia na matamanio yetu, kutafuta elimu, kutafuta kipato cha kuendesha maisha, kuilea familia, kuamrisha yaliyo mema na kukataza yaliyo mabaya, na kadhalika.

Katika vitabu vya historia na pia katika uandishi wa habari, neno '*Jihad* ' linatumiwa sana kwa kulihusisha na mapigano na vurugu. Haya ni makosa, kwa sababu mapigano kwa neno la Kiarabu ni '*Qital*' na sio '*Jihad*'. Imezuliwa kuwa Uislamu ulisambaa kwa upanga kwa jina la *Jihad*. Huu ni uzushi wa kiajabu kabisa ulio kaririwa sana katika vitabu vya historia; Uislamu ulitandaa katika dunia kwa sababu ya mafundisho yake ya busara na tabia njema za kibinadamu, sio kwa upanga; hakujapatapo kutokea katika historia ya Kiislamu Upiganaji wa Dini au Mahakama dhidi ya uasi wa dini, (*Crusade na Inquisition*). Neno la '*Vita Vitukufu*' (Holy War) halimo katika lugha (maneno) ya Kiislamu. Asili ya neno hili linatokana na Baba Urban wa Pili katika mwaka 1095 alipowataka Wakristo wote wa Uropa kujiunga katika "*Vita Vitukufu*" dhidi ya Waislamu ili kuirejesha ardhi takatifu (Holy Land, yaani Jerusalem). Bilashaka, Waislamu walipigana vita katika historia yao, lakini vita hivyo vilikuwa vya kuondowa uoneaji au kuondoa ukandamizaji na kuweka uhuru wa fikra na dini; kwa hakika vilikuwa vita vya kusimamisha uhuru, sio vita vya kulazimisha watu dini. Kwa mfano, Waislamu walitawala India kwa mamia ya miaka na hakupatapo

kutokea kampeni ya kuwalazimisha watu kuwa waislamu; mpaka hivi leo India imebakia vile vile kuwa na wafuasi wingi zaidi wa Kihindusi.

Maneno haya ya Kiingereza '*Jihadist*' na '*Jihadism*' ni maneno ya kisasa yanayotumiwa katika vyombo vya habari kuupa jina Uislamu wenye msimamo mkali au vikundi vya ugaidi na itikadi zao. Maneno haya ni uvumbuzi wa kisasa na hayana mizizi yoyote katika historia wala maana katika Uislamu.

Uislamu haujaruhusu uovu wowote wa vurugu. Waislamu wanaruhusiwa kupigana kwa kujikinga nafsi tu na kwa kuondoa uonevu. Katika hali hii kupigana huko kunaweza kuitwa Jihadi kwa sababu mtu anakuwa katika jitihadi ya kujikinga au kuondowa uonevu. Allah anasema katika Qur'ani 2:193;

> ***Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina, na sharia iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu.***



***Masjid Sultan Ahmed ni msikiti wa kihistoria uliopo Istanbul, Turkia. Bado watu wanasujudu katika salaa juu ya zulia jekundu la fahari hapo panapo adhiniwa kusali. Blue Mosque, kwa jina lake mashuhuri, ulijengwa baina ya mwaka 1609 na 1616 wakati wa utawala wa Ahmed Wa Mwanzo. Katika jengo lake la elimu limo kaburi la Ahmed, chuo na pahala pakupumzikia wasafiri.***

# Sharia katika Uislamu

Sharia (*Shari'ah* kwa lugha ya Kiarabu) ni **kanuni za maadili** zilizo kamilifu, zenye kuendesha maisha ya mwanadamu kwa kufuata yale atakayo Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa yaliyomo katika Sharia ni misingi ya imani, namna za kuabudu, tabia njema, kanuni za iktisadi na nidhamu ya hukumu (penal code). Maana ya neno '*Shari'ah*' ni 'muongozo au njia iliyo sawa', na kwa hiyo kwa Kiislamu ina maana ya 'njia ikupelekayo kwenye uokozi na mafanikio ya milele'. Kuwa Muislamu hasa ni kuishi kama inavyosema *Shari'ah* kwa sababu ndio njia ya kuishi alioweka Mwenyezi Mungu.

Asili ya *Shari'ah* ya Kiislamu inatokana na Qur'ani na sunna za Mtume. Ufafanuzi wa sharia na mahitajio mepya yanayotakiwa katika sharia hupatikana kwa rai za wataalamu wa kidini (kwa Kiarabu *ijma*').

Uamuzi na hukumu ya mwanadamu peke yake hauwezi kuweka



*Mahakama Kuu, Muscat, Oman*

maadili kwa wanadamu wote kwa njia ya haki na usawa. Kwa sababu ndani ya uamuzi wa mwanadamu kuna mapendeleo, chuki, majivuno, tamaa, maslaha ya nafsi, hisia, na udhaifu mbali mbali wa mwanadamu. Tunamuhitaji Muumba wetu kutuongoza na kutupa njia ya maadili ya haki na ya usawa wa kweli, na hii ndio *Shari'ah* ya Kiislamu. Nayo ni **kanuni ya maadili** rasmi yenye lengo la kuhifadhi maisha ya mwanadamu, heshima yake, akili, imani, familia na mali.

Mara nyingi *Shari'ah* hutajwa kwa kauli kali dhidi ya Uislamu ya kuwa ni sharia ya Kiislamu itowayo idhini ya kukandamiza wanawake, kuozesha watoto wadogo, kuzuia uhuru wa watu, na kadhalika. Aina hizi za kauli zinatokana na ujinga wa kutojua hasa ni nini *Shari'ah*; uhakika ni kuwa ni sharia ya Kiislamu inayopigana na uwovu unaotuhumiwa, na uwovu wote unaowasibu wanadamu. Kwa mfano, ni sharia ya Kiislamu iliyoweka kanuni na muongozo juu ya usawa wa kijinsi, haki za wazee na za watoto katika familia, haki za masikini na wenye kuhitaji, maadili ya vita na vipi kuwafanyia mateka, njia halali za kibiashara, ustahmilivu wa dini, adabu njema katika jamii, uongozi wa kiserekali, na kadhalika.

Ufuatao ni mfano wa aya za Qur'ani ambazo ni asili ya *Shari'ah* ya Kiislamu kuhusu haki na usawa katika biashara, (Qur'an 26:181-183).

أَوْفُوا۟ ٱلْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا۟ مِنَ ٱلْمُخْسِرِينَ ۝
وَزِنُوا۟ بِٱلْقِسْطَاسِ ٱلْمُسْتَقِيمِ ۝
وَلَا تَبْخَسُوا۟ ٱلنَّاسَ أَشْيَآءَهُمْ وَلَا تَعْثَوْا۟ فِى ٱلْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ۝

***Timizeni kipimo sawa sawa, wala msiwe katika wanao punja. Na pimeni kwa haki iliyo nyooka; Wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye jeuri kwa ufisadi.***

# Mgawanyiko katika Uislamu

Katika zama za Mtume na zama za viongozi watatu wa mwanzo (au Khalifa) baada ya kufa kwake, Waislamu walikuwa ni jamii moja, ingawaje kulikuwapo ufarikiyano katika uongozi, khasa wakati wa khalifa wa tatu (Uthman ibn Affan, 644-656 CE). Katika wakati wa khalifa wa nne (Ali ibn Abi Talib, 656-661 CE), mafarikiyano na upinzani wa kisiasa ulizidi. Ugomvi na vita viliyofuata vikasababisha kuzuka vikundi vitatu; waliokuwa wakimpiga vita Ali, waliokubaliana na mapatano baina ya Ali na wapinzani wake, na wale waliokuwa pamoja na Ali lakini walikataa mapatano na wapinzani wa Ali. Kwa hivyo, kwa kihistoria makundi katika jamii ya Waislamu yalikuwa juu ya kutafautiyana kisiasa na sio katika dini. Wakati huu ndipo uwendeshaji serekali na mambo ya Shari'ah yakaanza kuachanishwa. Wataalamu wa dini wengi wakachipuka katika makundi matatu hayo na kutowa fikra zao katika uwelewaji wa sharia na matumizi yake. Wanashariah wakubwa wakatokeza, kama: Jabir bin Zayd (639–709 CE), Abu Hanifa (699–767 CE), Ja'afar Sadiq (702-765 CE), Malik (711–795 CE), Shafi'i (767–820 CE), na Ibn Hanbal (780–855 CE). Kila mmoja katika wana chuoni hawa, ambao wanaitwa *Imam*, cheo cha heshima kwa kuwa na usomi mkubwa wa dini na sharia, walijenga nidhamu ya kutoa kanuni na uamuzi wa kisheria, na wakazungukwa na makundi ya wafuasi. Kufikia karne ya 10, mafundisho yaliyowekwa na wana chuoni hawa wakuu yakafanyika kuwa "Vyuo vya Kisharia" vilivyo jengeka, vikaendeshwa kwa utiifu wa wanavyuoni wake. Kwa hayo, chuo cha Jabir bin Zayd kikajulikana kwa jina la *Ibadhi*, cha Abu Hanifa kuwa *Hanafi*, cha Ja'afar Sadiq kuwa *Shia'*, cha Malik kuwa *Maliki*, cha Shafi'i kuwa *Shafi'i*, na cha Ibn Hanbal kwa jina la *Hanbali*. Kwa hakika kuchipuka kwa vyuo hivi ilikuwa sio niya ya maimamu sita hawa. Kupita karne tatu zilizofuata, Waislamu wa kawaida pia wakainukia kufuata chuo fulani katika vyuo hivi.

Juu ya kuwepo makundi ya vyuo hivi vya sharia, Waislamu wote ni

wamoja na wanaunganishwa na kitabu kimoja, Qur'ani, ambayo haikubadilika tangu kuteremshwa zaidi ya karne kumi na nne zilizopita, na pia kuunganishwa na sunna za Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye). Waislamu dunia nzima hawahitilafiani katika misingi ya imani na dini, na wanafanya ibada zao za kidini kwa umoja kama vile salaa na hija.

Inapasa kujuwa kwamba Uislamu unakataza mgawanyiko wa makundi katika dini. Allah anasema katika Qur'ani 3:103,

> ***Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane.***

Kwa kuishikilia amri hii, vyuo vyote vya kisheria vya Kiislamu vinaishi kama jamii moja na kustawi kwa karne nyingi. Mapigano ya kusikitisha kati ya Waislamu tuliyoyaona katika historia na ambayo yalitokea katika nyakati za karibuni, hayakuwa na uhusiano na dini kabisa, bali yalikuwa ni mapambano ya kisiasa na mamlaka za nchi.



***Msikiti wa Umayyad, unaojulikana pia kwa jina la Msikiti Mkuu wa Damascus, uliopo katika mji mkongwe wa Damascus, ni mmoja katika misikiti mikubwa na mikongwe duniani. Unachukuliwa na baadhi ya Wasilamu kuwa ni pahala pa nne patukufu katika Uislamu.***

# Haki za Mwanadamu katika Uislamu

Mwanadamu ameenziwa na kupewa hishima kubwa katika viumbe vya Allah. Allah anasema katika Qur'ani 17:70:

> ***Na hakika tumewatukuza wanaadamu, ... na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.***

Ili kuiweka na kuihifadhi heshima hii, Uislamu umeziasisi haki za lazima kwa wanadamu wote, bila ya kujali dini, kabila au cheo. Zifuatazo ni baadhi ya haki muhimu na za lazima katika Uislamu, kama ilivyo kaririwa katika Qur'an:

1. Utukufu wa roho ya binadamu na haki ya kuishi. Kuongezea juu ya aya 5:32 iliyotajwa katika Mlango wa 15, Allah anasema:

   > ***…Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini.... Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini. (Qur'an 6:151)***

2. Haki ya kupata mahitajio ya lazima ya kuendesha maisha. Ni wajibu kwa Waislamu kuhakikisha kuwa wanadamu wenzao wamepata mahitajio yao ya lazima.

   > ***Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba. (Qur'an 51:19)***

   Kusaidia masikini na kuwaangalia kihali wale wenye shida sio tendo la hisani au upendeleo, bali ni haki ya masikini na wenye shida.

3. Haki ya kuwa huru.

   > ***Je! Ameukata huo mlima (njia nzito ya kumfikisha Peponi).***

> ***Na nini kitakachokujulisha huo mlima? (Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana.(Qur'an 90:11-13)***

Utumwa una sura nyingi. Miongoni mwao ni utumwa wa kiwiliwli na wa kiuchumi, ufanyaji kazi wa kulazimishwa, kutumishwa kijinsi, na aina nyenginezo za kutumishwa kwa nguvu.

Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye) alisema:

> ***Kuna aina tatu za watu ambao mimi mwenyewe nitashitaki dhidi yao Siku ya Hukumu. Mmoja kati ya watatu hawa ni yule amfanyae mtumwa mtu aliye huru.***

Kwa hiyo, Uislamu ulipiga marufuku utumwa katika karne ya 7, hali ya kuwa utumwa ulipigwa marufuku nchi za Magharibi mwishoni mwa karne ya 19. [38]



***Msikiti Mkuu wa Xi'an, China. Uislamu ulifika China mwanzoni mwa karne ya 7. Leo kuna Waislamu zaidi ya milioni 20 katika China.***

4. Usawa wa wanadamu wote: Watu wote ni sawa na kiwango cha pekee cha ubora kwa Mwenyezi Mungu ni usafi wa moyo na tabia njema.

   ***Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari. (Qur'an 49:13).***

5. Haki ya uadilifu na usawa katika mambo yote ya jamii na ya kiiktisadi, bila ya kujali cheo cha mtu katika jamii.

   ***Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hata ikiwa dhidi ya nafsi zenu, au wazazi wawili na jamaa zenu. Na ikiwa (dhidi ya) tajiri au masikini Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuate matamanio, mkaacha kufanya uadilifu. Na mkiupotoa au mkajitenga nao basi Mwenyezi Mungu anajua vyema mnayo yatenda. Qur'an 4:135)***

6. Kuhifadhiwa kwa heshima, hadhi na faragha ya mtu.

   ***Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu. (Qur'an 49:11)***

   Na vilevile katika aya 49:12, Allah anasema:

***Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.***

7. Uhuru wa kusema ya haki na kukataza mabaya.

***Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu... (Qur'an 9:71)***

Na vilevile katika aya 4:148, Allah anasema:

***Mwenyezi Mungu hapendi uovu uenezwe kwa maneno ila kwa mwenye kudhulumiwa. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.***

8. Uhuru wa dini na uhuru wa mtu kufanya ibada yake. Waislamu wanaamini kwamba ni wajibu wao kuwajulisha watu ukweli wa Uislamu. Lakini, hakuna mwenye haki ya kumlazimisha yoyote kufuata imani yoyote, kwa kuwa imani ni kuamini kwa dhati na hiari katika nafsi ya mtu. Allah anasema katika Qur'ani aya 2:256,

***Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.***

Uhuru huu wa dini unakaririwa katika aya nyingi za Qur'ani.[39]

Mafundisho haya mema ya Kiislamu na mengine yaliokuwemo katika Qur'ani na Hadithi za Mtume yamekusudiwa kwa wanadamu wote na ni msingi wa haki za binadamu na demokrasi.

# Anuwai za Utamaduni katika Uislamu

Uislamu unatambuwa kuwepo kwa hitilafu katika tabia, kabila, lugha, kivazi, chakula, fani, mila na dhahiri nyenginezo za kitamaduni. Na haya sio halali tu, bali ni katika neema za Allah. Lakini, Uislamu haukubali na unakataza mambo katika utamaduni yanayokwenda kinyume na mafundisho na nguzo zake. Allah anasema;

> ***Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi. (Qur'an 30:22)***

Katika aya nyengine, Allah anasema;

> ***Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari. (Qur'an 49:13).***

Katika ulimwengu wa sasa uliotandaa, watu hawakosi kuziona tafauti dhahiri katika Waislamu watokao kwenye makabila na utamaduni mbali mbali. Hapa huwa muhimu kutafautisha baina ya kilicho cha utamaduni na kilicho cha dini, na uhusiano (au uingiliano) baina ya dini na utamaduni ili kuweza kufahamu tafauti zilizopo ndani ya ulimwengu wa Waislamu.

Uislamu unajitokeza na kuonekana kwa sura mbali mbali katika tamaduni mbali mbali za ulimwengu. Hili sio lakushangaza, kwa sababu Uislamu ni dini ya ulimwengu na imetapakaa kila pembe ya dunia na kuchanganyika na tamaduni mbali mbali. Lakini sura zote hizi za Uislamu zina asili ile ile moja ya mzizi wa imani na dini ya Kiislamu. Kwa mfano, Waislamu wote wanamuamini Mungu mmoja. Wote wanaamini kuwepo kwa malaika.

Wote wanaisoma na kuifuata Qur'ani moja. Wote wanamuamini Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye). Wote wanaamini akhera na kuhisabiwa siku ya hukumu. Wote wana imani ya Uamuzi wa Mwenyezi Mungu na Majaaliwa Yake. Nguzo tano za Uislamu zinatekelezwa na Waislamu wote duniani sawa sawa. Mwito wa salaa (*adhana*) ni ule ule, uwepo Oman au Indonesia au Senegal au China. Waislamu wote duniani wanafunga pamoja katika mwezi wa Ramadhani na wanakusanyika Makka pamoja wakati wa ibada ya kila mwaka ya kuhiji. Kwa hivyo, katika Uislamu kuna umoja katika asili ya imani na dini, juu ya kuwepo hitilafu za kitamaduni.

Kwa hivyo dini lazima huchanganyika na utamaduni, kwa sababu utamaduni unajengeka kwa mafunzo na tabia njema zinazotokana na dini inayofatwa na jamii ya watu. Kwa hivyo, hakuna dini isiyo changanyika na utamaduni, na hakuna utamaduni usio changanyika na dini.[40] Changamoto kubwa kabisa kwa Waislamu (na wasiokuwa Waislamu), ni kutafautisha baina ya mafundisho na kanuni za Kiislamu na ufasiri wa kitamaduni ambao mara nyingi huwekwa juu ya mafundisho hayo na kanuni hizo. Hata Mtume Muhammad alitambua na kutarajia kuwa Waislamu mwishowe watapambana na hali ambazo hazikuelezewa katika Qur'ani na Sunna. Daima patakuwepo hali mpya za kitamaduni na za kisheria ambazo zitahitaji uchambuzi wa makini, na akili za wana sharia wenye ujuzi na hisia. Hapana shaka, patakuwepo na masuala mapya katika majimbo mbali mbali ya dunia na zama zake, ambayo ni mbali kabisa na yale yaliyokutwa wakati wa Mtume, na kwa hivyo, ufasiri na kujibu masuala ya kitamaduni yanayo chipuka ni kazi ambayo Waislamu wamekuwa wakipambana nayo daima.

Kwa kawaida wachunguzi, khasa wale wanaotoka nchi za Magharibi, huwa na mitizamo miwili wanapo zipima jamii za Waislamu na kujaribu kuzifahamu. Mtazamo wa kwanza, Waislamu wanaonekana kuwa ni jamii moja isiobadilika. Popote walipo, Waislamu wote ni sawa, bila

ya kuhusisha na tafauti za nchi au zama.[41] Mtizamo huu haujali tafauti dhahiri za kitamaduni katika ulimwengu wa Waisalmu. Mtizamo wa pili unahitilafiana kabisa na ule wa mwanzo. Uislamu umetengana na vitabu vyake na badala yake kutambulikana kwa wafuasi wake. Ilivokuwa Waislamu ni watu wa aina mbali mbali, basi pia kuna "Uislamu aina nyingi", kama Uislamu wa Kiturki, Uislamu wa Kilibnani, Uislamu wa Kiomani, Uislamu wa Kiindonesia na kadhalika. Kwa mujibu wa mtizamo huu, hakuna ulimwengu mmoja wa Uislamu, bali kuna ulimwengu wa "Uislamu aina nyingi".[42] Hapa, ule mpaka wa hitilafu ya utamaduni umepanuliwa hadi ya kuugawa Uislamu kufuatana na utambulishi wa kitaifa. Mtizamo uliyo sahihi ni kuwa Uislamu ni dini moja inayojengeka ndani ya tabiya za utamaduni mbali mbali bila ya kutengana na mafundisho asasi ya Qur'an na Sunnah za Mtume. Hali zamaisha fulani, na matatizo na changamoto za wakati fulani, yanawapelekea Waislamu kutafuta cha kuwaongoza kutoka kwenye Qur'ani na Sunnah. Kwa hivyo dini na mahitajio ya watu huleta fahamu mpya na tafsiri pana ya maandishi yale yale asili yasiobadilika.[43] Uislamu ni mmoja lakini una sura mbali mbali za kitamaduni.

Tukimuangalia Muislamu binafsi, Uislamu wake unategemea kiwango chake cha ujuzi wa mafundisho, kiwango chake cha kufahamu mafundisho hayo na undani wake, na kadiri ambayo mafundisho hayo anavyoyatekeleza. Kadhalika, Uislamu wa kila jamii una athari za hali, wakati na pahala palipo hiyo jamii.

Kwa hivyo Uislamu ni dini moja yenye sura nyingi zilizo jitokeza katika nafsi na utamaduni mbali mbali. Tafauti hii ni ushahidi kuwa Uislamu ni dini ya walimwengu wote na dini inayo patana na tamaduni zote bila kuachana na nguzo zake na mafundisho yake. Waislamu wanaona uzani huu kama ni ushahidi wa hekima na rehema za Mwenyezi Mungu. Uislamu unapatana sana na tamaduni, na daima huikuza na kuiendeleza tamaduni. Lakusikitisha ni kwamba baadhi ya Waislamu wanasahau au

wanashindwa kuyaunga mambo ya kitamaduni na mizizi yao ya Uislamu, ama kwa sababu ya dharau tu au ukosefu wa kujua historia. Yanapotokea hayo, mazoweya ya kitamaduni ambayo yapo kinyume na mafundisho ya Uislamu huweza kukua na kuonyesha kuwa ndio Uislamu.[44] Kuna matendo mengi mabaya kama hayo ya kitamduni ambayo yanaonekana katika baadhi ya jamii za Kiislamu, ambayo kwa makosa, huambatanishwa na Uislamu au kuwa yanatokana na mafundisho ya Kiislamu. Kwa mfano, kuozeshwa mwanamke kwa nguvu, kuozeshwa watoto wadogo, mauaji ya kuweka heshima, ubora wa kuzaa mwanamume, na kutahiri wanawake, yote haya ni kinyume na mafundisho ya Kiislamu na yanaleta sura mbaya kwa Uislamu.



*Msikiti Mkuu wa Kilwa Kisiwani, Tanzania. Uislamu ulianza kusambaa katika mwambao wa Africa Mashariki na visiwa vyake tokea karne ya 7. Kilwa ilistawi kama ni dola ya Kiislamu kwa karne nyingi mpaka ilipo vamiwa na Wareno mwaka 1505 CE ambao waliteketeza utamaduni na majenzi makuu ya dola hii na kuuwa iktisadi yake. Waomani waliwatowa Wareno Afrika Mashariki yote mwisho wa karne ya 17. Msikiti Mkuu wa Kilwa Kisiwani uliasisiwa karne ya 10 na kupanuliwa na masultani waliofwatia katika karne ya 11 na 12 .*

# Kwanini Dini ni Muhimu?

Kuna sababu sita za umuhimu wa dini:

1. Maadili yetu, tabia na vitendo vyetu hutokana na kile tunachokiamini kuwa ni kawaida ndani ya nyoyo zetu. Kawaida hii inatokana na utamaduni tunaourithi. Kawaida ya kitamaduni imejengeka kwa athari ya dini na imani ya utamaduni huo. Bila ya kuwepo kawaida ya kitamaduni, mwendo wa maisha yetu utababaishika, tusijuwe tunapoelekea, na kuvunjika kwa maadili na kawaida kama invyotambulika na jamii, na haya huleta mvurugano ndani ya jamii na pia ndani ya kila nafsi. Kwa hivyo, dini ni muhimu kwa sababu ndio yenye kujenga imani ambayo inajenga kawaida yetu ya kitamaduni na mtazamo wetu wa dunia. Dini ndio dhamana inayo hakikisha uzima wa jamii na nafsi za kila mtu.

2. Dini ndio msingi pekee wa kupata maarifa kuhusu Mwenyezi Mungu: Yeye ni Nani, nini sifa Zake na vipi umbile Lake? Kwa hiyo, dini ni muhimu kwa sababu kuikana dini ni sawa na kumkana Mwenyezi Mungu.

3. Dini ndio msingi pekee wa maarifa kuhusu mambo ya hakika na kweli tusioyaona. Dini ndio ambayo inatueleza juu ya umbile la milele la roho ya mwanadamu, kuwepo uhai baada ya kufa, kuwepo kwa Malaika na venginevo. Kwa hiyo, bila ya dini mtu huwa hatambui na hajuwi kabisa mambo ya kweli na hakika ambayo hatuyaoni na yamekiuka uwezo wa hisia zetu.

4. Dini ndio yenye kutueleza juu ya lengo la maisha yetu: Kwa nini nipo hapa? Mwishowe nitakwenda wapi? Nini yatakuwa matokeo ya yale niliyoyachagua katika uhai huu? Watu wengi wanakata tamaa katika maisha na wamo katika hali ya majonzi kwa sababu ya kutokua na maarifa juu ya lengo la maisha.

5. Dini maana yake ni njia na namna ya kuishi; nidhamu ya kuendesha maisha yenye kusudio la kuihami na kuihifadhi heshima ya mwanadamu

na usalama wake, pia kuweka hali zenye kuleta maisha ya mapatano na ya furaha. Dini ndio yenye kuweka viwango sawa vya tabia njema na nidhamu sawa ya haki katika maisha. Kupuuza dini kunapelekea kwenye orodha yote ya maovu ya mwanadamu; unyonyaji, dhulma, uonevu, tamaa, ubaguzi, ufisadi na mengi mengineo. Dini ni muhimu kwa faida ya jamii.

6. Na mwishowe, dini ni muhimu kwa sababu inatuambia vipi kujitayarisha na maisha yetu yajayo. Kama ilivyo elezwa katika Mlango wa 9, uhai baada ya kifo ni hakika na kilichopo huko mbele kinategemea na maamuzi yetu tunayoyafanya katika uhai huu. Dini inatuambia kwa yakini ni nini Mwenyezi Mungu Muumba anachokitarajia kwetu, vipi kuendesha maisha yetu na nini yatakuwa matokeo ya vitendo vyetu huko akhera.

Maisha bila ya dini ni maisha yaliyokosa lengo la kuishi na yaliyokosa fahamu kubwa ya kuwepo hapa duniani, pia ni maisha yasiyoona ya mbele. Si jambo la busara kuisukuma dini pembeni, kama aya hii ya Qur'ani inavyotutahadharisha:

> ***Na kwa waliomkufuru Mola wao Mlezi ipo adhabu ya Jahannamu. Na ni marejeo maovu yalioje hayo! Watakapo tupwa humo watausikia mngurumo wake na huku inafoka. Inakaribia kupasuka kwa hasira. Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni mwonyaji? Watasema: Kwani! Ametujia mwonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa! Na watasema: Lau kuwa tungeli sikia, au tungeli kuwa na akili, tusingeli kuwa katika watu wa Motoni! Wakakiri dhambi zao. Basi kuangamia ni kwa watu wa Motoni! Hakika wanao mwogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu, watapata maghfira na ujira mkubwa. (Qur'ani 67:6-12)***

# Vipi kuingiya katika Uislamu?

Uislamu umejengeka kwa nguzo sita za imani na nguzo tano za dini ambazo zimeelezwa katika Mlango wa 2 wa kitabu hiki. Mtu anapozifahamu na kuzikubali nguzo hizi anaingiya katika Uislamu kwa kutamka kwa dhati yafuatayo:

***Ash'hadu an laa ilaaha illa Allah wa ash'hadu anna Muhamada Rrasuulullah.***

***Nashuhudia kuwa hakuna anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wa Allah.***

Kauli hii kwa Kiarabu inaitwa *Shahada*, maana yake ni ahadi na uhakikisho juu ya imani. Kwanza hutamkwa kwa Kiarabu na halafu kwa lugha anyoifahamu huyo anayeingiya katika Uislamu.

Baada tu ya kutamka *Shahada*, Muislamu mpya anawajibika kutekeleza kwa imani na vitendo nguzo za imani na za dini.

Mtu asiye Muislamu anapoukubali Uislamu, basi kwa hakika huwa anarejea katika "dini yake ya uzazi", kwa sababu kila mtu amezaliwa kwa maumbile yaliyo katika hali ya kujisalimisha kamili katika Amri ya Allah na anazaliwa na hisia ya utu wema asili, (kwa Kiarabu *fitrah*). Baada ya kuzaliwa na kupata umri, kinachomuelekeza mtu kufuata dini fulani ni wazee wake na utamaduni aliokulia nao. Kwa hivyo ni wajibu wa mtu mwenyewe kuutafuta ukweli na kufuata lililo la mantiki na lenye kuingia akilini katika mambo ya imani na dini.

## Ukweli wa Imani

1. Imani pofu yenye msingi wa sudfa ya kuzaliwa katika aila fulani na kufuata mababu hua sio imani ya kweli.

2. Imani ya kweli ni lazima iwe na msingi wa maarifa, akili na mantiki.

3. Msingi wa imani ya mtu ni lazima ujengeke na uthibitisho mzito.

**Muhtasari:** Katika Uislamu, imani na akili sio vitu mbali mbali visivyohusiana. Mtu anatakiwa aitumie akili kuthibitisha na kuiiamirisha imani yake.

# Orodha ya Maneno

**Allah:** Jina binafsi na khasa la Mwenyezi Mungu Muumba na Mlezi wa Ulimwengu. (Tazama Mlango wa 3)

**Ayah:** Aya yoyote katika Qur'ani. Pia ina maana ya "Ishara za Mwenyezi Mungu"

**Khalifa:** Kiongozi wa jamii ya Kiislamu. Pia '*Khalifa*' ni neno la Kiarabu lenye maana ya 'mwakilishi'.

**Hadith:** Hadithi au Sunnah ni kauli na mifano ya vitendo vya Mtume Muhammad (Salaa na amani za Allah zimfikiye). Kwa pamoja mafundisho haya yanaitwa 'Sunnah za Mtume'. (Tazama Mlango wa 8).

**Hajj:** Kuhiji Makka kwa Waislamu kila mwaka. (Tazama Mlango wa 2)

**Hijra:** Kuhama kwa Waislamu kutoka Makka kwenda Madina katika mwaka 622 CE. Mwaka huu ndio mwanzo wa kalenda ya Kiislamu inayoitwa 'Kalenda ya Hijra'. (Tazama Mlango wa 4) .

**Ibadhi:** Moja kati ya Vyuo vya Kisheria vya Uislamu. (Tazama Mlango wa 18).

**Islam:** Jina la dini yenye kuhubiri imani juu ya Upekee wa Mwenyezi Mungu Muumba, Allah, na kukubali na kujisalimisha kamili katika Amri Zake. (Tazama Mlango wa 2) .

**Jihad:** Kujitahidi kwa bidii katika kumtii na kumtumikiya Allah. Kila tendo la muumini linalofanywa kwa kusudio la kupata ridhia na kibali kwa Allah ni *Jihad*. (Tazama Mlango wa 16).

**Ka'bah:** Nyumba ya mwanzo kujengwa ulimwenguni kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja. Nyumba hii imo ndani

ya uwanja wa msikiti mkubwa wa Makka, na kwa kawaida hufunikwa na kitambaa cheusi.

**Madinah:** Ni mji katika Saudi Arabia uliopo kiasi cha kilomita 400 kaskazini ya Makka. Hapa ndipo ulipo msikiti wa pili mtukufu katika Uislamu, Msikiti wa Mtume, (kwa Kiarabu *Masjid Al-Nabawi*) .

**Makkah:** Mji uliopo sehemu za magharibi ya Saudi Arabia. Hapa ndipo palipo Ka'ba na msikiti wa mwanzo mtukufu katika Uislamu. (kwa Kiarabu unaitwa *Masjid Al-Haraam*) .

**Muislamu:** Mtu mwenye kuamini na kufuata mafundisho ya dini ya Kiislamu.

**Qibla:** Mwelekeo wa Makka ambao Waislamu huelekea katika Salaa.

**Qur'ani:** Ujumbe wa mwisho wa Mwenyezi Mungu alioteremshiwa Mtume Muhammad. (Tazama Mlango wa 6) .

**Shari'ah:** Nidhamu ya maadili ya Kiislamu ambayo imo ndani yake misingi ya imani, namna za kuabudu, tabia njema, mafundisho ya kijamii na ya iktisadi na nidhamu ya hukumu. (Tazama Mlango wa 17)

**Shia':** Moja kati ya Vyuo vya Kisheria vya Uislamu. (Tazama Mlango wa 18)

**Sunni:** Moja kati ya Vyuo vya Kisheria vya Uislamu. (Tazama Mlango wa 18)

**Surah:** Sura (au mlango) katika Qur'ani.

**Ummah:** Jamii ya Waislamu wote katika ulimwengu wa Waislamu.

# Tanbihi

1. Kila yanapotajwa majina ya mitume, Waislamu huwaombea kwa Allah kwa kusema: " Salaa na amani za Allah zimfikiye au ziwafikie". (Tazama pia Qur'ani 33:56, 37:181)

2. Qur'ani 2:132, 136, 22:78

3. Nguzo za imani zinatajwa katika aya nyingi za Qur'ani, kwa mfano; 2:3-4, 2:285, 4:136, 54:49, na nyenginezo.

4. Ni dhahiri katika Qur'ani kuwa vitendo vyetu havikuamuliwa kabla na Mwenyezi Mungu. Kwa mfano tazama aya 4:62, 10:44, 13:11, 18:29, 30:41, na nyenginezo.

5. Nguzo za dini zinatajwa katika aya nyingi za Qur'ani, kwa mfano; 2:3, 2:43, 2:183, 2:196, 3:97, 22:78 na aya nyenginezo.

6. Maana ya Taqwa ni kuogopa au kijikinga. Ina maana ya jitihadi katika kujikinga na ghadhabu ya Allah na kuogopa na kuwa na hisia ya uwangalifu wake juu yetu. Jitihadi hii ndio inayomfanya mtu awe mchamungu, mwenye kufanya mema na kukataza maovu.

7. Qur'ani 7:158, 21:107, 33:40, 34:28. Ujumbe wa Mtume unawawajibikiya Majinni vilevile.

8. Hili toleo la ukubwa lilifanywa na Utbah bin Rabia'h (baba mkwe wa Abu Sufyan) ambaye alikuwa katika waheshimiwa wa Makka.

9. Qur'ani 29:50-51

10. The Holy Qur'an, Translation and Commentary, by A. Yusuf Ali, The Islamic Foundation, London, 1975. Tafsiri ya aya 7:157.

11. Qur'ani 3:3, 4:47, 5:48, 15:9, 26:192-196, 76:23, na aya nyengine.

12. Uhusiano wa mtu na Allah na viumbe vyote vilivyobakia unatajwa

katika aya nyingi za Qur'ani. Kwa mfano; 1:2, 2:21-22, 2:257, 7:54, 50:21, 82:10-12, 18:50, 6:112, 12:5, 6:38, 2:164, 31:10, 36:71-73.

13. Qur'an 2:38-39, 2:81-82, 17:9-10, na aya nyengine.

14. Qur'an 3:137, 10:71–73; 11:25–49, 12: 1–113, 17:2-8, 71:1–28.

15. Kitabu "The Geological Concept of Mountains in the Qur'an", El-Naggar, Ukurasa wa 5.

16. Ukitaka kusoma zaidi juu ya mada hii, rejelea vitabu hivi: (1) Qur'ani & Modern Sciences, by Dr. Zakir Naik, (2) The Bible, The Qur'an and Science, by Maurice Bucaille, (3) The Qur'an: Unchallengeable Miracle, by Caner Taslaman, translated by Ender Gurol.

17. Qur'ani 2:34, 17:61

18. Qur'ani 14:44-46, 74:8-10, 80:33-46

19. Qur'ani 13:22-23, 36:55-56, 52:21

20. Qur'ani 5:48, 16:36, 10:47

21. Qur'ani 3:64–65; 3:98–100, 4:47, na aya nyengine.

22. Qur'ani 2:75, 2:79, 2:146, 159, 174, 3:71, 4:46, 5:13 na 5:15. Wanavyuoni wa Biblia wenye asli ya Ukristo pia wanathibitisha ukweli huu, kwa mfano tazama (1) 'Misquoting Jesus' na (2) 'Jesus Interrupted' by Bart D. Ehrman.

23. Qur'ani 5:48.

24. Qur'ani 11:118-119

25. Qur'ani 3:59, 4:171, 5:75, 5:116-117, 19:30,

26. Biblia (KJV); Matheo, 24:36, Yohana 5:30, 14:28, 17:3 na 20:17, Matendo 2:22. Kusoma zaidi katika mada hii (kwa lugha ya

Kiingereza) fungua anwani hii katika mtandao: http://www.islam-guide.com/ch3-10-1.htm. Kadhalika unaweza kusoma (kwa lugha ya Kiingereza) 'The First and Final Testament', kiloandikwa na Dr. Lawrence Brown.

27. Qur'ani 3:45, 4:171, 5:72, 19:30.

28. Qur'ani 19:27–33 na Qur'ani 3:49; 5:110.

29. Qur'ani 5:110 na 57:27.

30. Biblia zote zinashuhudia juu ya uhakika wa kuwa Yesu, (Salama na baraka za Allah zimfikie), alitumwa kwa "Watoto wa Israel" tu. Kwa mfano, tazama (KJV), Matheo 10:5-6 na Matheo 15:22–26.

31. Miongoni mwa wana sayansi alikuwa Sir Antony Flew aliyekuwa mfuasi mkuu wa Ukanaji Mungu. Katika mwaka 2004 alitangazia imani yake ya kuwepo kwa Mungu, na katika mwaka 2007 aliandika kitabu cha anuani – "There is God: How the World's Most Notorious Atheist Changed His Mind", (Mungu Yupo: Vipi Mkanusha Mkuu wa Mungu amebadilisha maoni yake).

32. Qur'ani 7:172 na 30:30

33. Qur'ani 3:86, 10:9, 13:27, 17:97, 18:17, 48:4, 74:31.

34. Qur'ani 17:70, 23:115, 29:2, 30:8

35. Ifuatayo ni mifano ya maovu yaliyowasibu wanawake katika historia: (1)Uarabuni kabla ya Uislamu, watoto wachanga wakike walikuwa wakizikwa wangali hai. (2) Warumi waliwafanya wanawake kama ni watumwa, na Wayunani (Greeks) waliwafanya wanawake kama bidhaa. (3) Ufaransa katika mwaka 587 CE uliitishwa mkutano wa kujadiliana na kuamuwa kuwa 'hali wanawake ni wanadamu au si wanadamu'. (4) Uingereza kabla ya mwaka 1850 wanawake

hawakuwa wakihisabiwa kuwa ni wananchi, na hawakuwa na haki zozote mpaka mwaka wa 1882. (5) Katika utamaduni wa China wanaume sio tu wakiruhusiwa kuwauza wake zao bali wakiruhusiwa hata kuwazika wangali hai. (6) Uhindusi ulichukulia wanawake kuwa ni dhara kushinda kifo, kuwa motoni, sumu au moto.

36. Qur'ani 2:190, 2:193, 2:217, 4:75 na 8:39

37. Qura'ni 8:67-70. Sehemu kubwa ya sura ya 8 na 9 (na kadhalika sura nyengine), zinazungumzia juu ya hali za kuingia kwenye vita, maadili ya vitani, sharia zenye kuhusu suluhisho katika vita, wenye kujisalimisha, namna ya kusimamia ngawira ya vita, utendeaji wa mateka wa vita. Ni muhimu kukumbuka kuwa Waislamu ndio wa mwanzo katika historia kuleta kanuni kuhusu utendeaji wa mateka.

38. Tazama historia ya kupigwa marufuku utumwa Katika: http://en.wikipedia.org/wiki/Abolition_of_slavery_timeline

39. Qur'ani 10:99, 109:1–6 na aya nyengine.

40. Marejeo ya Vitabu, 6, Ukurasa wa 183

41. Marejeo ya Vitabu, 7, Ukurasa wa 4

42. Marejeo ya Vitabu, 7, Ukurasa wa 4

43. Marejeo ya Vitabu, 8, Ukurasa 110-114

44. Marejeo ya Vitabu, 8, Ukurasa 116-118

# Marejeo ya Vitabu

I. The Holy Qur'an, Translation and Commentary, by A. Yusuf Ali, The Islamic Foundation, London, 1975.

II. Towards Understanding The Qur'an, by Sayyid Abul A'la Maududi, The Islamic Foundation, London, 1992.

III. Qur'an and Modern Sciences: Conflict or Conciliation? By Dr. Zakir Naik (2008), Islamic Research Foundation, Mumbai, India.

IV. Ulum Al-Qur'an, An Introduction to the Sciences of the Qur'an. By Ahmed Von Denfer, The Islamic Foundation, London, 1983

V. Muhammad in the Hindu Scriptures. By Dr. Ved Prakash Upaddhay, Published by A.S. Noordeen, Malaysia, 2007

VI. Tariq Ramadan, Radical Reform: Islamic Ethics and Liberation, Oxford University Press, Oxford, 2009.

VII. Clinton Bennet, Muslims and Modernity: An Introduction to the Issues and Debates, Continuum, New York, 2005.

VIII. Mehmet Ozalp, Islam between Tradition and Modernity, Barton Books, Australia, 2012.



*"Ar-Rahmaan", Mwingi wa Rehema. Hii ni moja katika sifa za Mwenyezi Mungu.*

# Ukumbusho

# تعريف الإسلام باللغة السواحلية



Mfumo wa Masi ya DNA ya chembe

Kitabu hichi hakiuzwi